SportPesa
TZS. 482,274,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#



**Mauaji** na unyama vyatikisa, askari Suma JKT mbaroni

UKURASA 2&3



**Barca yamtaka Koeman kuwatumia Puig, Umtiti**

UKURASA 21


# Nipashe

Jumatano Septemba 8, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580697

MWANGA WA JA…

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US




# Biashara watoto wauzwa 30,000/-

• **Wadaiwa** kupelekwa kwa wafugaji... *Endelea Uk. 2*

## YALIYOMO


**UKURASA WA 5**
**KANISA KATOLIKI LAONYA MADAKTARI**
RAIS wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas...

**UKURASA WA 5**
**JELA MIAKA 10 KUMFANYIA UKATILI WA KINGONO MTOTO**
MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Igunga, mkoani...

**UKURASA WA 7**
**SERIKALI KUAMUA 'TUITION' SHULENI**
OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa...




Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akitazama viatu alipotembelea banda la kiwanda cha Kilimanjaro International Leather Industries Company Limited kilichoko Karanga, Moshi, kabla ya kufungua mkutano wa wadau wa sekta ya mifugo kwenye Kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Julius Nyerere, Dar es Salaam, jana. Wa pili kulia ni Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki. **PICHA: PMO**

## Upelelezi tukio la Hamza kuvuka mipaka

UKURASA 3



Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi.



Katibu Mkuu wa Chadema, John Mnyika.

## CHADEMA yamjibu msajili wa vyama, naye atoa neno

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA YAITAKA TUSKER IKIISUBIRI MAZEMBE** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Biashara watoto wauzwa 30,000/-

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATU wawili wanashikiliwa na Jeshi la Polisi mkoani Mbeya kwa tuhuma za kuwatorosha watoto kwenye maeneo mbalimbali na kuwasafirisha kwenda kuwauza kwa wafugaji, ili wakatumike kuchunga mifugo.

Akizungumza na waandishi wa habari jana katika Kituo cha Kikuu cha Polisi jijini hapa, Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Daniel Julius (21) mkazi wa Kijiji cha Nsonga na Kamungu Julius (30) mkazi wa Kijiji cha Rwimba wilayani Mbarali.

Kamanda Matei alisema watuhumiwa walikamatwa Septemba 5, mwaka huu wakiwa na watoto 11, ambao wana umri wa kati ya miaka 10 na 14. Alisema watuhumiwa waliwatorosha baadhi ya watoto hao kutoka kwa wazazi wao na wengine ni wale wanaoishi kwenye mazingira magumu.

Alisema watuhumiwa hao walikuwa wanawauza watoto hao kwa wafugaji walioko wilayani Mbarali kwa gharama kati ya Sh. 25,000 na 30,000.

"Askari wetu walipata taarifa za siri kuhusu biashara hiyo haramu ya binadamu na ndipo wakaanza kuweka mitego kwenye maeneo mbalimbali ya Wilaya ya Mbarali ndipo walipowakamata watuhumiwa wakiwa na watoto hao wakitaka kwenda kuwauza," alisema Kamanda Matei.

Alisema watuhumiwa hao mbali na kuwauza watoto hao, pia walikuwa wanawatumikisha kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji wakati wakiendelea kutafuta wateja wa kuwauza.

Baadhi ya watoto hao, alisema walichukuliwa kwa kushawishiwa na wengine waliokuwa wanachukuliwa kwa nguvu na kusafirishwa kwa kutumia pikipiki kwenda maeneo, ambayo watuhumiwa walikuwa wanawahifadhi.

Alisema kati ya watoto hao 11, wawili walitambuliwa mapema na wazazi wao na wakachukuliwa, hivyo akawataka wazazi, ambao wamewahi kupotelewa na watoto kwenda katika kituo kikuu cha polisi cha mkoa kwenda kuwatambua.

Matei aliwatahadharisha wafugaji wilayani Mbarali na maeneo mengine ya mkoa kuacha kuwatumikisha watoto kwenye shughuli za kuchunga mifugo kwa maelezo kuwa watakumbana na mkono wa sheria.

"Tunaendelea kufanya upelelezi, ili tujue na wengine, ambao wamekuwa wakishirikiana na watuhumiwa hawa na tukishakamilisha upelelezi wetu, tutawafikisha watuhumiwa mahakamani kwa hatua zaidi za kisheria," alisema.

Katika hatua nyingine Kamanda Matei alisema Jeshi hilo linamshikilia Abdala Joseph (21) mkazi wa Lupa akiwa na slaha aina ya bastola ambayo anaimiliki kinyume cha sheria na kwamba alikuwa anajiandaa kwenda kuifanyia uhalifu.

Alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa na askari waliokuwa doria juzi katika kituo cha mafuta cha Kazi Bure kilichoko katika mji mdogo wa Mbalizi.

Alisema mtuhumiwa baada ya kuhojiwa alikiri kuwa amekuwa akifanya matukio mbalimbali ya uhalifu katika mkoa huo na hivyo Jeshi hilo litamfikisha mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.



Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, akizungumza baada ya utiaji saini wa mkataba wa ushirikiano kati ya wizara na TANESCO wa ujenzi wa miundombinu ya mkongo wa taifa wa mawasiliano kwa kutumia umeme. Kulia ni Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani na kushoto ni Mwenyekiti wa Bodi ya TANESCO, Dk. Alexander Kyaruzi. Wapili kushoto ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Zainabu Chaula. **PICHA: WMTH**

# CHADEMA yamjibu Msajili

**Maulid Mmbaga na Patson Andugalile** (TUDACO)

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) kimemjibu Msajili wa Vyama vya Siasa nchini, Francis Mutungi, kuhusu kauli yake ya kuvizuia vyama kufanya mikutano kuwa ni ukiukaji wa sheria na kanuni za vyama vya siasa.

Jaji Mutungi, mwanzoni mwa wiki alivitaka vyama vya siasa nchini kusimamisha makongamano na mikutano ya kisiasa kwa muda ili kupisha mazungumzo baina ya vyama hivyo, Polisi na Ofisi ya Msajili ili kutafuta suluhu ya mikutano na makongamano.

Akizungumza jana ofisi za makao makuu ya CHADEMA, Kinondoni mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi wa Mawasiliano, Itikadi na Mambo ya nje wa chama hicho, John Mrema alisema, kauli ya Msajili haikuzingatia sheria hivyo hawako tayari kuitii.

"Tunatumia nafasi hii kumkumbusha Msajili wa Vyama ambaye ni Jaji wa Mahakama Kuu kuhusu kauli yake kwamba, hana mamlaka ya kisheria kusimamisha shughuli za vyama vya siasa ambavyo vipo kwa mujibu wa sheria.

"Lakini vilevile tunamkumbusha Msajili kwamba badala ya kusimamisha shughuli za vyama zinazofanyika kwa mujibu wa sheria na Katiba ya nchi, anapaswa amuonye na amkanye Mkuu wa Jeshi la Polisi aache kuingilia shughuli halali za vyama vya siasa," alisema Mrema.

Mrema alisema kuwa kwa kauli yake Msajili anaendelea kuvunja sheria na Katiba ya nchi huku akitolea mfano kuwa siku chache zilizopita mkoani Mara RPC alizuia kongamano la kudai Katiba mpya la CHADEMA, akidai kuwa sasa ni wakati wa kujenga uchumi.

Alisisitiza kuwa vyama vya siasa vinatimiza wajibu wake kwa mujibu wa Katiba.

"Ibara ya 26, 1 ya Katiba inasema, 'kila mtu ana wajibu wa kufuata na kutii katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano, msajili wa vyama naye anawajibu wa kufuata na kutii katiba hii na sheria za vyama, hivyo hawezi kuzuia shughuli za vyama eti mpaka tukutane na polisi," alisema Mrema.

Alidai kuwa msajili anapaswa kufahamu kwamba ibara ya 147 ya Katiba kifungu kidogo cha tatu na nne kimepiga marufuku kwa majeshi yote kujihusisha na vyama vya siasa, na kunukuu kifungu cha tatu kinachosema; "Itakuwa ni marufuku kwa mwanajeshi yeyote kujiunga na chama chochote cha siasa isipokuwa tu atakuwa na haki ya kupiga kura iliyotajwa katika ibara ya tano ya katiba hiyo".

"Kifungu cha nne cha ibara hii kinatoa tafsiri kwamba 'kwa madhumuni ya ibara hii mwanajeshi ni askari aliyeajiriwa kwa masharti ya muda au ya kudumu katika Jeshi la Ulinzi la Polisi, Magereza au la Kujenga Taifa" kwa hiyo kauli ya Msajili aliyoitoa anavunja Katiba," alisema Mrema.

"Wito wetu kwa Msajili wa Vyama vya Siasa amuandikie barua rasmi Mkuu wa Jeshi la Polisi amkanye na kumuonya aache kuvunja Katiba na sheria ya vyama vya siasa kwa kuingilia shughuli halali za vyama nchini.

"Pili tunamtaka Msajili Jaji Mtungi arudi akasome Katiba, sheria ya vyama vya siasa na kanuni zake ambazo zinavipa vyama haki na uhuru wa kufanya mikutano ya hadhara, maandamano na vikao vya ndani badala ya kujiingiza kuendelea kuvunja sheria ya vyama, aache kuinajisi Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa," alisisitiza Mrema.

**MSAJILI AFAFANUA**

Katika taarifa iliyotolewa jana kwa vyombo vya habari, Jaji Mutungi alisema baadhi ya vyama vimepotosha taarifa yake, aliyoitoa juzi.

"Katika mkutano wangu nilieleza kinagaubaga azma yangu ya kuitisha kikao maalum cha wadau wa siasa kutafuta suluhu ya mivutano iliyojitokeza baina ya jeshi la polisi na vyama vya siasa, hususan vyama vinapotaka kufanya makongamano, mikutano ya ndani.

"Kwa masikitiko nimebaini baadhi ya wadau, kwa sababu wanazozijua wao aidha kwa makusudi au kwa kutokuelewa vizuri, wanapotosha taarifa hiyo, kwa kudai kuwa nimetoa amri ya kusitisha mikutano ya ndani ya vyama vya siasa. Hilo halina ukweli wowote na niwasihi mlipuuze kwa uzito unaostahili," alisema.

Jaji Mutungi alisema, hajatoa amri ya kuzuia bali amevishauri vyama vya siasa katika kipindi wanachojaribu kupata ufumbuzi wa mivutano ni busara ya kawaida "wakati jitihada zikiendelea vyama vijizuie kwa muda kuendelea na shughuli zilizosababisha kutokea kwa mivutano hiyo."

## Akutwa ameuawa na kukatwa miguu

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKAZI wa Kijiji cha Daki, Chemba mkoani Dodoma, Rashidi Ndwata (40), amekutwa ameuawa kwa kunyongwa shingo na kisha miguu yake kutenganishwa na kiwiliwili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Onesmo Lyanga, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akitoa taarifa ya matukio mbalimbali kwa waandishi wa habari.

Alisema tukio hilo lilitokea juzi saa 6:30 usiku na kwamba mtu huyo aliuawa kwa kunyongwa shingo, kuchomwa na kitu chenye ncha kali shavu la kulia, kupigwa na kitu kizito kwenye taya la juu na chini.

"Kisha kukatwa miguu sehemu ya chini ya magoti na mwili wake kufunikwa na mahindi yaliyokwisha kupukuchuliwa na kuchomwa moto,"alisema Kamanda Lyanga.

Alisema chanzo inadaiwa ni mgogoro wa ardhi kati ya marehemu na ndugu zake na kwamba hadi sasa watu wanne wamekamatwa kwa mahojiano zaidi kuhusu tukio hilo.

"Uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa wauaji baada ya kufanya tukio hili walichukua mahindi yaliyopukuchuliwa na kufunika mwili wa marehemu na kuchoma moto ambao uliendelea kuwaka hadi pale wanafunzi walipokuwa wakipita asubuhi nyumbani kwa marehemu na kuona moto unawaka na kutoa taarifa kwa viongozi na baadaye kwa jeshi la polisi," alisema.

Kadhalika Kamanda Lyanga, alitoa rai kwa wananchi kuacha kujichukulia hatua mkononi bali wafuate taratibu za kisheria ili kupata haki zao.

"Ziko njia nyingi za kutatua migogoro ya ardhi ikiwamo mabaraza ya ardhi ya wilaya. Kama mtu unaona umepokonywa haki yako basi ziko mahakama pia unaweza kwenda kutoa malalamiko yako na si kujichukulia sheria mkononi," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, jeshi hilo limewatangazia wote walioomba nafasi za kujiunga na taasisi hiyo kupitia Kamanda wa polisi mkoa kuwa wanatakiwa kufika ofisi za wakuu wa polisi wa wilaya (OCD) katika maeneo yao au ofisi ya kamanda wa mkoa kwa ajili ya kuona wenye sifa ambao wataendelea na usahili kuanzia Septemba 13 hadi 18, mwaka huu.

# Upelelezi wa tukio la Hamza kuvuka mipaka

**Na Romana Mallya**

JESHI la Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam limesema upelelezi dhidi ya tukio la Hamza Mohammed, ni endelevu kwa sababu makosa ya ugaidi yanahusisha nchi zaidi ya moja.

Kaimu Kamanda wa Kanda hiyo, Daniel Shillah, aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Nipashe iliyotaka kufahamu mpaka sasa nini kinaendelea dhidi ya kesi hiyo na ni watu wangapi wanaendelea kushikiliwa.

Kuhusu walioshikiliwa mpaka sasa, Kamanda Shillah alisema wanapoona mtu hausiki wanamwachia.

Hata hivyo, Shillah hakutaka kutoa ufafanuzi zaidi kuhusiana na upelelezi wa tukio nje ya Tanzania.

"Tunashikilia watu watatu au wanne na huenda baadaye tukawaachia wote kulingana na upelelezi unavyokwenda, hatuwezi kuwaachilia mtu mmoja halafu tukaita waandishi wa habari," alisema.

Tukio la Hamza kushambulia askari na kuua wanne na kujeruhi watu wengine sita lilitokea wiki mbili zilizopita katika eneo la Selander, jijini Dar es Salaam.

Hamza akiwa na silaha awali aliwashambulia askari wawili waliokuwa kwenye kibanda chao maeneo hayo ya Selander kisha akachukua silaha zao mbili aina ya pistol na kuanza kurusha ovyo risasi na kusababisha vifo vingine viwili vya askari na kuwajeruhi watu sita.

Mauaji hayo yalitokea wakati Hamza akirushiana risasi na polisi karibu na Ubalozi wa Ufaransa ambapo polisi walimuua na ndipo baadhi ya ndugu zake akiwamo mama na wadogo zake waliposhikiliwa na Jeshi la Polisi kwa mahojiano na baadhi yao kuachiwa na wengine kuendelea kubaki.

Waliouawa katika tukio hilo ni askari watatu wa Jeshi la Polisi na mmoja kutoka kampuni ya ulinzi binafsi.



Rais wa shirikisho la wachimbaji madini nchini (FEMATA), John Bina (katikati), akizungumza na wafanyakazi wa mgodi wa dhahabu wa JB Gold, uliopo Dutwa wilayani Bariadi, mkoani Simiyu juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mtoto akutwa amekufa ndani ya pagale

**Na Christina Mwakangale**

MTOTO Angel Mwakajonga mwenye umri wa miaka sita mkazi wa Mtaa wa Igale Kata ya Forest jijini Mbeya, amekutwa amefariki dunia na mwili wake kutupwa kwenye pagale jirani na nyumba aliyokuwa akiishi na bibi yake.

Taarifa iliyoifikia Nipashe jana kutoka mkoani Mbeya na kuthibitishwa na ndugu na jamaa ilibainisha mshtuko wa tukio hilo baada ya mama mzazi kushuhudia mwili kwenye maeneo ya pagale majira ya asubuhi baada ya kumtafuta usiku kucha.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, aliithibitishia Nipashe kutokea kwa tukio hilo.

Dada wa marehemu, Cecy Mwakajonga, alisema mwili wa mdogo wake ulibainika umetupwa kwenye pagale hilo baada ya bibi yake kumtafuta tangu juzi usiku majira ya saa 1:00 usiku bila mafanikio.

"Sasa hivi tupo msibani hapa nyumbani, bibi alimtafuta jana (juzi) usiku baada ya kuona hajarudi nyumbani. Asubuhi katika kutafuta tunashangaa mwili hapo jirani na nyumbani," alisema Cecy.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Forest, Mary Majwanga, alisema alipata taarifa ya tukio hilo jana asubuhi na kwamba taarifa alizopata baada ya kufika msibani ni kwamba mtoto huyo alitafutwa usiku wa jana (juzi) bila kupatikana.

"Bibi wa mtoto huyu alinipigia simu saa 4:00 usiku akisema mtoto hajarudi akidhani atapatikana akiwa mzima na hata utafutaji wake haukuwa wa sana. Asubuhi leo (jana) saa 2:00 asubuhi kumuuliza amepatikana akasema bado.

# Askari SUMA JKT wadaiwa kuua

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WALINZI watatu wa Shamba la Wakala wa Taifa wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mbegu za Kilimo (ASA), ambao ni askari wa Shirika la Uzalishaji Mali la Jeshi la Kujenga Taifa (SUMA JKT), wanadaiwa kusababisha kifo cha mkazi wa Ngaramtoni, Arumeru mkoani Arusha.

Askari hao wanadaiwa kusababisha kifo cha Almasi Mohamed na kuwajeruhi watu wengine watatu kwa kipigo wakiwatuhumu kuiba mahindi.

Jana, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Kamishna Msaidizi (ACP) Justine Maseju, alisema askari hao wanashikiliwa na jeshi hilo kwa mahojiano zaidi kuhusiana na mauaji hayo.

"Ni kweli tunawashikilia askari watatu wa SUMA JKT na upelelezi unaendelea kuhusu tukio hili la mauaji na tutatoa taarifa rasmi baada uchunguzi kukamilika," alisema.

Kabla ya Polisi kuthibitisha taarifa za mauaji hayo, mke wa marehemu, Mwanahamisi Rajabu, alisema mumewe kabla ya kufariki dunia juzi alikuwa na majeraha kutokana na kipigo na alilazwa katika Hospitali ya Olturumet akiwa anatapika damu.

"Nilipigiwa simu na polisi kuwa mume wangu amelazwa hospitalini anaumwa sana kutokana na kipigo. Nikaenda na kumkuta ana hali mbaya na akanieleza kwa taabu kilichotokea na baadaye akafariki (dunia)," alisema.

Alipotafutwa kuzungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kitongoji cha Seuli, Elias Ndemlya, alisema marehemu wakati wa uhai wake alikuwa mkazi wa eneo hilo na mkulima ambaye awali alikuwa mfanyakazi wa shamba hilo.

"Hili si tukio la kwanza kwa askari wanaolinda shamba hilo kupiga watu na kujeruhi, wakiwatuhumu ni wezi. Tunaomba Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi (George Simbachawene), kutafuta mwarobaini wa matukio haya licha ya watuhumiwa kupelekwa mahakamani kujibu tuhuma zinazowakabili," alisema.

Kwa mujibu wa Mwenyekiti huyo, majeruhi wengine wawili waliopigwa na askari hao na kisha kuteswa kwa kuburuzwa, wamelazwa katika Hospitali ya Olturumet.


JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA
ILIYOPO DAR ES SALAAM

SHAURI LA MAOMBI YA MADAI NA. 508/18 LA 2018

A-ONE PRODUCTS AND BOTTLERS LTD…………..MWOMBAJI

DHIDI YA

ABDALLAH ALMASI NA WENZAKE 15………………..WARUFANI

KWA: (1) ABDALLAH ALMASI (2) ODOLO KYAHE (3) SAIDI MAGOMA (4) ZUHURA YUSUF (5) HALIMA HAYUNI (6) SALUM YAHAYA (7) LUCY MWAMI (8) MOHAMED HAJI (9) ILAILA NAMPOKELA (10) MOHAMED KANIKI (11) JANETH ANTHONY (12) SECILIA MAGELLA (13) PRIMITIVA KAHIGI (14) MWANAIDI OMARY (15) HADIJA SALUM (16) ASUMANI HUSSEIN

POPOTE MLIPO.

Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa tarehe 21/9/2021 saa tatu kamili asubuhi (3:00) katika Mahakama ya Rufani, Tanzania ikiketi Dar es salaam. Mnatakiwa kufika bila kukosa wenyewe au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria. Pia msipofika wenyewe au wawakilishi wenu, shauri hili litasikilizwa bila ya uwepo wenu.

*Imetolewa leo hii tarehe 02 Mwezi Septemba, 2021.*

THE COURT OF APPEAL OF TANZANIA

D. R. LYIMO
Kny: MSAJILI
MAHAKAMA YA RUFANI (T)

116445902

MAHOJIANO MAALUM -2

# Mwenyekiti PAC aguna ufanisi wa Deni la Taifa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

KILA mwaka unapoingia na kutoka, mipango na mikakati ya serikali ni 'chanda na pete'. Kukopa na kulipa Deni la Taifa nako kumekuwa kukisikika wakati wa kusomwa kwa makadirio ya bajeti ya serikali kwa mwaka husika.

Hata hivyo, bado kuna utata unaoendelea kuwa mjadala kuhusu manufaa ya Deni la Taifa.

Katika sehemu hii ya pili ya mazungumzo kati ya Nipashe na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, binafsi anajenga hoja kwa kuweka kiulizo kikubwa kwa mustabali wa deni hilo.

**Endelea**...



Mwenyekiti wa PAC, Naghenjwa Kaboyoka.

**SWALI**: Deni la Taifa linazidi kupaa. Tufanye nini kama nchi kukabiliana na hali hii japo serikali imekuwa ikisisitiza bado ni himilivu?

**KABOYOKA**: Kwa kuwa serikali ndiyo ina takwimu za uchumi na inasema deni ni himilivu, hatuna jinsi. Madeni yanapozidi kukua maana yake hela yako ya nchi inazidi kulipa madeni haya, hivyo unakosa hela nyingi za kufanyia kazi za maendeleo.

Na hii ndio sababu fedha kwa ajili ya maendeleo nchini ni kidogo. Unapotoa mishahara ya watumishi na madeni, unabakiwa na kidogo sana.

Kwa hiyo, tunajidai kwamba deni linahimilika lakini kupata fedha za maendeleo ni vigumu kwa sababu kila inapofika wakati kwamba deni limeiva, inabidi ulipe.

Kwa hiyo, makusanyo yetu yanazungukia kwenye kulipa madeni, kulipana mishahara na kugharamia huduma ndogo kama za elimu na afya ambazo hazizalishi. Na hata zikizalisha, ni baada ya muda mrefu sana.

Matokeo yake kupiga hatua kimaendeleo sisi itakuwa ngumu sana kwa sababu hela ya maendeleo unapeleka kulipa madeni.

Ni kama baba wa familia, ukiwa na madeni mengi huwezi kuwekeza hata kwenye biashara.

Tunasema Deni la Taifa linahimilika lakini linatugharimu sana kulipa riba pale deni linapokuwa limeiva.

**SWALI**: Ipo hoja ya Halima Mdee katika hili kwamba turuhusu taasisi za kimataifa zije zitufanyie tathmini ya kifedha ili tuwe tunakopa kwa masharti nafuu tu badala ya masharti ya kibiashara. Wewe unasemaje?

**KABOYOKA**: Shida kubwa ipo kwenye mkataba kati yao na Wakala wa Ndege za Serikali. Ule mkataba ndio umekaa vibaya kiasi kwamba utaendelea kuipa hasara ATCL.

ATCL kupewa ndege za kukodi na Wakala wa Ndege za Serikali sio jambo baya, lakini mkataba wa kusema kwamba ATCL kila mwezi wapeleke hela za matengenezo.

Yaani mkataba unawataka wapeleke hela kama advance (malipo ya awali) kwa ajili ya matengenezo makubwa ya zile ndege ili ikifika wakati huo wa matengenezo kuwe na hela.

Hata hivyo, unapofika wakati huo wa matengenezo, kunakuwa hakuna zile hela kutoka kwa Wakala wa Ndege za Serikali.

Matokeo yake ni kwamba ATCL inabidi watumie tena hela zao kwenda kutengeneza ndege wakati wameshapeleka fedha za matengenezo kwa wakala.

Sasa unaona kwamba unatumia mtaji wao kwa ajili ya matengenezo ya ndege wakati fedha yao imeshafungwa kule.

Unatumia mtaji wako kutoa fedha nyingine kwa ajili ya kupeleka tena ndege kutengenezwa.

Mbaya zaidi, mkataba unasema ukifika muda wa kama mwaka mmoja hivi zile fedha unazozipeleka kwa Wakala wa Ndege za Serikali huzipati tena. Zile hela hazirudi. Sasa ukiangalia, ni mikataba ya aina gani hii? Pia angalia ndege zilizopo wanazotumia ATCL.

Zile ndege za masafa marefu wamekosa kibali cha kuingia kwenye hizo nchi.

Shida ni nini? Wanaogopa zitakamatwa kwa sababu wanadaiwa. Sasa kwa kukosa safari za masafa marefu, hizi ndege kubwa zinatumia mafuta mengi sana.

Ukiruka kwa masafa mafupi ni hasara kubwa sana. Hela yote uliyopata inaishia kwenye mafuta tu, huna faida wala nini.

Hizi ndege kubwa zilipaswa kuzisaidia zile ndogo kiuendeshaji. Kwa hiyo, ni hasara kubwa kuwa na ndege hizi.

Kama nchi itamaliza madeni yake, hizo ndege zikapata hayo masafa marefu, ATCL inaweza kufanya kazi kwa faida.

Lakini serikali isipomaliza kulipa madeni yake inayodaiwa na wadau mbalimbali huko nje, ina maana kwamba hizi ndege zitaendelea kufanya hasara. Sasa maana ya kuwa na ndege hizo hizo ni nini? Ndipo shida ilipo.

Kwa kuwa serikali imenunua ndege hizi, tena kwa pesa taslimu, haina budi kulipa madeni ili zitengeneze faida. Kama ndege hizi zingekuwa za kukodi, unazirudisha kwa wenyewe. Unawaambia 'jamani biashara imenishinda, ninarudisha ndege zenu'.

Lakini tumezinunua cash (kwa fedha taslimu), hivyo tumejifunga wenyewe maana hatuna wa kumrudishia.

Njia pekee tulipe madeni yetu huko nje tunayodaiwa ili tupate zile safari ndefu za kwenda huko Uingereza, Ujerumani, Afrika Kusini, China.

**SWALI**: Mlikumbana na vikwazo vingi wakati wa kushughulikia sakata la mkataba wa Kampuni ya Lugumi na Jeshi la Polisi. Je, PAC imekumbana na vikwazo vipi katika kushughulikia Ripoti ya CAG kwa mwaka 2019/20?

**KABOYOKA**: Kwa sasa hakuna vikwazo, hatuna vikwazo tena. Kwenye kamati kwa sasa sioni kikwazo chochote kinachotufanya tushindwe kufanya kazi.

Mheshimiwa Spika ametupa uhuru mkubwa kwamba kile tutakachosema ndiyo hicho hicho. Hatuna yule anayesema 'hiki hapana'.

Hata wakati ule wa uongozi wa Hayati Rais John Magufuli, alisema waziri yeyote akiwaambia 'ooh hiki hapana, kule tumeambiwa hakihojiwi, niambieni nitalifanyia kazi'.

Watu wengine walikuwa wanatumia mbinu hiyo kuifumba macho kamati au baadhi ya wajumbe wa kamati kwamba 'jamani hili Rais hataki', kumbe wanasema kwa manufaa yao wenyewe.

Sasa, Mheshimiwa Spika ameshasema 'hapana, kamati fanyeni kazi yenu kwa uhuru. Ndiyo maana umeona hata TPA (Mamlaka ya Bandari) tumewarudisha,

TASAC tumewarudisha na wale wengine tuliona hawajatosheleza, warudi kwanza hadi pale tutakapotembelea mashirika yao tuone wanachofanya.

**SWALI**: Je, mapendekezo yenu kuhusu mkataba kati ya Kampuni ya Lugumi na Jeshi la Polisi yamefanyiwa kazi.

**KABOYOKA**: ... (kicheko) Ni swali ambalo siwezi kujibu kwa maana sina kigezo cha kufanya tathmini kuhusu suala hilo kwa sasa.

Mpaka CAG (Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali) aende aone kama yamefanyiwa kazi au hayajafanyiwa kazi kisha atuletee ripoti kama wamefunga ile mitambo.

CAG hajaenda. Kama akienda atuletee ripoti kwamba kweli mitambo imefungwa au kuna kazi imefanyika kwa kiwango fulani.

# TEC yawaonya madaktari mgonjwa kutolewa nyuzi

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

RAIS wa Baraza la Maaskofu Katoliki Tanzania (TEC), Askofu Gervas Nyaisonga, amewataka madaktari nchini kujiepusha na mienendo inayochafua maadili ya taaluma zao.

Alitoa angalizo hilo kwenye ufunguzi wa mkutano mkuu wa 84 wa mwaka wa Chama cha Madaktari wa Kikristo Tanzania (TCMA) uliofanyika jijini hapa.

"Juzi niliona video ya daktari kamshona mgonjwa, lakini inadaiwa kuwa baada ya kukosa fedha alimfumua nyuzi huyo mgonjwa, bahati nzuri siyo wa hospitali zetu za dini ya Kikristo, hivyo tuwe na huruma kwanza bila kujali maslahi ya fedha,' alisema Askofu Nyaisonga.

Alisema madaktari wanapaswa kujitoa kuokoa maisha ya watu badala ya kutanguliza maslahi ya fedha.

"Mnatakiwa kuwa na huruma pamoja na kujiepusha na vitendo vya rushwa wakati wa kuwahudumia wagonjwa wanaofika kupata huduma za afya kwenye maeneo yenu, kazi ya kuwahudumia wagonjwa ni kazi ya wito, hivyo wanapaswa kufanyakazi kwa moyo wa kuthamini maisha ya binadamu na kujituma bila kushawishika au kuwa na tamaa ya kujinufaisha," alisema.

Askofu Nyaisonga alisema madaktari wamepewa dhamana ya kutunza afya za watu, hivyo wanatakiwa kuzingatia maadili ya kazi yao na wajitume katika kuokoa maisha ya watu na kuwataka kuzingatia viapo vyao.

Aidha, alishukuru serikali kwa kuendelea kuruhusu na kushirikiana na mashirika ya dini zote nchini katika kuanzisha na kutoa huduma za kijamii hasa afya.

Rais wa chama hicho, Dk. Bwire Chirangi, alisema mkutano huo unajumuisha madaktari zaidi ya 300 kutoka vituo, zahanati na hospitali za makanisa yote nchini.

Alibainisha kuwa mashirika hayo ya dini yanachangia kwa kiwango kikubwa huduma za afya na ustawi wa jamii kuna hospitali 105, kwamba kati ya hizo 38 ni teule za halmashauri na 10 zimepewa hadhi ya rufaa ya ngazi ya mkoa.

Dk. Chirangi aliongeza kuwa mashirika hayo yanamiliki zahanati 720 na vituo vya afya 100 kote nchini, wanaendesha baadhi ya vyuo vya mafunzo ya uuguzi na madaktari pamoja na vyuo vya kufundisha wataalamu wa ngazi mbalimbali za afya.

Baada ya tukio hilo wilayani Korogwe, mkoani TRanga, Waziri wa Afya, Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Doroty Gwajima, ameshatoa maelekezo ya kumsimamisha mtumishi huyo pamoja na kuagiza mabaraza ya huduma za afya kufanya uchunguzi wa tukio hili na kumkabidhi taarifa ndani ya siku 10.



Wanafunzi wa darasa la saba wa Shule ya Msingi Atlas, wakiandaa madawati na kubandika namba shuleni hapo, Madale mkoani Dar es Salaam jana, kwa ajili ya mitihani yao ya kumaliza elimu ya msingi inayoanza leo. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Onyo udanganyifu mtihani darasa la 7

**Na Romana Mallya**

WAKATI watahiniwa 1,132,143 wanatarajia kuanza leo mtihani wa kumaliza darasa la saba, Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA), limeonya walimu wakuu, waratibu wa elimu kata na wamiliki wa shule kutojihusisha na vitendo vya udanganyifu.

Katibu Mtendaji wa NECTA, Dk. Charles Msonde, alitoa onyo hilo jana mkoani Dar es Salaam wakati akizungumzia kuhusu mitihani hiyo inayotarajia kufanyika nchini kwa siku mbili kuanzia leo.

Dk. Msonde alisema utafiti wa baraza hilo umeonyesha chanzo cha udanganyifu katika shule ni baadhi ya walimu wakuu na baadhi ya waratibu wa elimu kata kupanga njama kutekeleza kufanyika udanganyifu sambamba na wamiliki wa shule.

"Baraza linawataka kwa dhati wasimamizi wakuu walioteuliwa na baraza mwaka huu, wasimamizi wa kuu wa shule kuhakikisha kwamba udanganyifu na njama zozote zinazohusu ndani ya vyumba vya mitihani zinadhibitiwa.

"Baraza halitasita kumchukulia hatua msimamizi mkuu yeyote niliyemteua atakayeshindwa kudhibiti udanganyifu ndani ya vyumba vya mitihani wakati mitihani ikiendelea."

Pia alisema baraza litawachukulia hatua walimu wakuu wa shule, waratibu wa elimu kata na wamiliki wa shule watakapobaini uwapo wao unachangia njama na kutekeleza udanganyifu kutokea katika maeneo yao.

Kadhalika, Dk. Msonde alitoa wito kwa wadau wengine kama ambavyo wamekuwa wakitoa ushirikiano kwao, watoe taarifa kwao pale wanapobaini kuna kikundi cha watu wanapanga njama za kujihusisha na udanganyifu.

"Milango ya baraza ipo wazi, tunawaomba wananchi wafanye vile vile wanavyofanya kila mwaka kujulisha mamlaka kuhusu wale wanaofanya udanganyifu ili wadhibitiwe," alisisitiza.

Dk. Msonde alifafanua kuwa kituo kimoja cha kufanyia mitihani kisipokuwa salama kinasababisha vingine vyote kutokuwa usalama.

"Vinaweza kusababisha athari ya kuhujumu uchumi wa nchi kwa sababu mtihani mmoja ukihujumiwa, mfano shule ya msingi, zaidi ya Sh. bilioni 79 zinatumiwa kwa hiyo kituo kimoja kisipokuwa salama ni kuhujumu uchumi wa nchi," alifafanua.

Alisema ndiyo maana wanasema pale mwenyekiti wa shule anapopanga njama za kutekeleza lazima wafute.

# Jela kwa kumfanyia ukatili wa kingono mtoto

**Na Jumbe Ismailly,** IGUNGA

MAHAKAMA ya Hakimu Mfawidhi wa Wilaya ya Igunga, mkoani Tabora imemhukumu Eva Timptheo (27), kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka 10 jela baada ya kumtia hatiani kwa kosa la kumfanyia vitendo vya ukatili wa kingono mtoto wa jinsia ya kike mwenye umri wa miaka minne.

Awali, Mwendesha Mashtakaa wa Jeshi la Polisi, Wilaya ya Igunga, Alex Kataya, alidai mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Julai 19, 2021.

Mbele ya Hakimu wa Wilaya ya Igunga, Godfrey Rwekiti, Kataya alidai katika tarehe hiyo na muda huo, mshtakiwa Eva Timotheo, alimfanyia kitendo cha ukatili wa kingono mtoto wa jinsi ya kike mwenye umri wa miaka minne kwa kumuingizia kitu butu kwenye sehemu zake za siri na na kumsababishia maumivu makali.

Alidai pia kwamba mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo kinyume na kifungu 138 C (1) (2) (b) kanuni ya adhabu sura ya 16 mapitio ya 2019 inayozuia kutenda makosa kama hayo.

Hata hivyo, mshtakiwa huyo baada ya kusomewa shtaka alikana na upande wa mshtaka ulipeleka mahakamani mashahidi sita akiwamo muathirika wa tukio hilo ikiwa ni pamoja na vielelezo na mashahidi wote walimtambua mshtakiwa.

Baada ya mahakama kusikiliza ushahidi wa pande zote mbili, Hakimu Rwekiti alisema ushahidi uliotolewa na upande wa mshtaka bila kuacha shaka yoyote ile umemuona mshtakiwa huyo, ana hatia na mahakama hiyo kumhukumu adhabu ya kifungo cha miaka kumi jela.

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Vyama vya siasa, polisi kukutana ni hatua nzuri*

**KATIKA** siku za karibuni kumekuwapo na hali isiyo rafiki katika tasnia ya kisiasa nchini.

Hali hiyo inatokana na kuibuka kwa malumbano na mivutano kati ya baadhi ya vyama vya siasa dhidi ya Ofisi ya Msajili na Jeshi la Polisi ambapo vyama vinazilalamikia taasisi hizo mbili kuwa hazivitendei haki.

Vyama hivyo ambavyo ni vikubwa vimekuwa vikidai kuwa taasisi hizo mbili zinavikandamiza badala yake zinakipendelea Chama Cha Mapinduzi (CCM) kama chama tawala hususan katika suala la mikutano ya ndani.

Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani aliruhusu vyama vya siasa kufanya mikutano ya ndani, lakini hivi karibuni vyama vya siasa vimekuwa vikilalamikia Jeshi la Polisi katika maeneo kadhaa nchini kuizuia mikutano ya ndani.

Hata hivyo, hakuna sababu rasmi zinazotolewa na makamanda wa jeshi hilo kuhusiana na uamuzi wake wa kuikataza mikutano hiyo wala kueleza ni mamlaka zipi zimetoa maagizo hayo.

Kadhalika, baadhi ya vyama vimekuwa vikitoa malalamiko dhidi ya Ofisi ya Msajili kwamba haivitendei haki, jambo ambalo kimsingi, limekuwa ikionyesha dalili mbaya kwa taasisi zetu kwa umma.

Tunaona hivyo kwa kuwa malumbano na majibishano kati ya wanasiasa wa upinzani na taasisi hizi za umma, kila uchao yamekuwa yakiibua mijadala mbalimbali ikiwamo kwenye mitandao ya kijamii, huku wananchi wakitoa kauli mbalimbali.

Mtazamo wetu ni kwamba hali hii inalitia doa taifa letu ndani nan je ya nchi yetu katika suala zima la haki za binadamu, demokrasia na utawala bora, hivyo kuwapo haja ya kuweka mambo sawa.

Hata hivyo, tumefarijika kusikia taarifa kwamba Ofisi ya Msajili wa vyama vya siasa, vyama vya siasa na Jeshi la Polisi likiongozwa na Mkuu wa Jeshi hilo (IGP), Simon Sirro, wanatarajia kukutana katika mkutano wa maridhiano.

Taarifa hiyo iliyotolewa na Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi juzi, ilieleza kwamba lengo la mkutano huo ni kuweka sawa namna ya kuendesha shughuli za kisiasa nchini bila kukwaruzana.

Jaji Mutungi akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, alisema lengo pia ni kujadili namna ya kuondoa kile kinachoonekana kwamba upo uhasama kati ya Jeshi la Polisi na vyama vya siasa pamoja na namna ya kuweka vizuri utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa.

Kwa upande wetu tunaona kuwa hatua ya kuitishwa kwa mkutano wa maridhiano ni nzuri na muhimu kwa afya ya taifa letu, ambalo limekuwa na utulivu mkubwa tangu baada ya kurejeshwa kwa mfumo wa vyama vingi vya siasa.


Pamoja na hatua hii kuchelewa, tunampongeza Jaji Mutungi kwa kueleza ukweli wa mambo kwamba mvutano kati ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi, limeanza kujenga taswira hasi kwa umma.

Hivyo basi tunamshauri Jaji Mutungi kuweka mazingira bora na rafiki ili pande husika ziaminiane badala ya kwenda kulumbana badala ya kufuta taswira iliyopo kwa umma.


Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




Na Sabato Kasika

## Muungwana Lazima Nilonge

# *Wanawake watumie njia hii kupenya waufikie uongozi*

**WANAWAKE** nchini wamekuwa mstari wa mbele wakihamasishana kujikita katika siasa, ili kuwania nafasi mbalimbali za uongozi, kwa kuwa wana uwezo wa kuongoza, pia kusaidia kukuza uchumi wa nchi yao.

Hiyo inatokana na ukweli kwamba, moja ya mambo ambayo wanaharakati wa kutetea wanawake, wamekuwa wakipiga vita kuona wengi wao wakiachwa nyuma katika kuwania nafasi za uongozi kwenye vyombo vya uamuzi.

Kuna sababu wanazozitaja kuwa ni chanzo cha kuwafanya wawe nyuma, ikiwamo vitendo vya rushwa vinavyofanywa na baadhi ya wanasiasa, kwa kuwageuza mtaji hasa kwenye kampeni za uchaguzi.

Wapo wanasiasa wanaowapa wanawake vitu kama khanga na vyakula, ili wawapigie kura, badala ya wao wenyewe kinamama kuwania nafasi za uongozi.

Ni mtindo unaokemewa na baadhi ya wadau wa siasa, kwa kuwa unawakwamisha wanawake kushika nafasi za uongozi na kubaki kuwa wapigakura, badala ya kuongoza.

Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGP), ni miongoni mwa wadau ambao wamekuwa wakipinga wanawake kutumika kupiga kura, badala ya kuwania nafasi za uongozi, ili idadi yao iwe sawa na ya kinababa.

Kuwapo kwa mtindo huo ni sawa na udhalilishaji wanawake. Hivyo, ni vyema ikaachwa haraka, ili kuwapa huru kuwania nafasi za uongozi na siyo kushawishiwa kwa vitu vidogo kama kuchagua badala ya kuchaguliwa kwenye uchaguzi.

Ushirikishwaji wa wanawake katika shughuli za kimaendeleo, ni muhimu kuongezewa msukumo zaidi, ili kuwajenga katika kujikomboa badala ya kutumika tu huku wakibaki nyuma.

Bahati nzuri, Rais Samia Suluhu Hassan, ameliona hilo na sasa anaendelea kulifanyia kazi, ili kuhakikisha kila mwanamke mwenye sifa za uongozi, ama anateuliwa au kuchaguliwa.

Msisitizo wake ni kwamba, anazingatia sifa na vigezo bila kujali mwanamke anatoka chama gani cha siasa, ila jambo la msingi kuangalia ni kama ana mchango kwa maendeleo ya taifa lililopo.

Ni kweli kwamba wapo watu wanawake na wanaume wenye uwezo wa kuongoza, lakini bahati mbaya wanakwama kupata nafasi hizo, kutokana na sababu mbalimbali, zikiwamo zinazodaiwa na wadau ni ukosefu wa fedha za kuwawezesha hatua za kuwashawishi wajumbe ndani ya vyama.

Itakuwa hatua nzuri, iwapo vyama vya siasa vitakuwa chachu ya kuwezesha wanawake wengi zaidi kupata uongozi, huku njia mojawapo ya kufikia hilo ni ikiwa ni kupanua wigo kwa kuwaruhusu kuwania uongozi bila vikwazo.

Kama ambavyo wanawake wanaharakati wenyewe wamekuwa wakiwa katika mtazamo uongozi siyo mzigo, kwamba mtu anapewa kuubeba kichwani, bali ni uwezo wa kuongoza. Hivyo, ni vyema vyama vikaendelea kuwawezesha.

Ni hatua ikakayowawezesha wajulikane, pia itakuwa rahisi kuonekana, hata kufikia hatua ya kuteuliwa na kiongozi wa nchi katika nafasi mbalimbali, kulingana na jinsi anavyotaka.

Katika dhana ya usawa kijinsia, baadhi ya wanawake wenye uwezo wa kuongoza wamekuwa wakiogopa kupambana ndani ya vyama au kwenye majimbo kutokana na hali duni ya kiuchumi.

Lakini, wakipewa nafasi na kuwezeshwa kiuchumi, njia hiyo inaweza kuwafanya wapate uongozi na hatimaye kufikia kile ambacho wamekuwa wakikitaja. Yaani kinachoitwa 'asilimia 50 kwa 50.'

Mazingira yanapokuwa rafiki, inakuwa rahisi kwa kufikia usawa wa kijinsia, ambao kwa muda mrefu wamekuwa wakiutamani, ili nao watoe mchango kwa mapana ya maendeleo ya nchi kwa ujumla.

Binafsi ninaamini, kupanua wigo wa uongozi au kuteuliwa kwa wanawake wengi katika vyama, ni sawa na kuunga mkono juhudi za Rais za kutaka kuhakikisha wenye uongozi wa uongozi wanateuliwa.

HABARI KITAIFA

# Sheria ya kulinda taarifa binafsi usafirishaji binadamu yapitishwa

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali Na. 5 wa Mwaka 2021, ambao pamoja na mambo mengine, unalenga kumpa mamlaka kila mtu kumfikisha kituo cha polisi kilicho karibu mshukiwa wa biashara ya usafirishaji wa binadamu.

Mbali na kurekebisha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, muswada huo, pia unapendekeza kufanyika marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, Sheria ya Ajira na Uhusiano wa Kazi, Sheria ya Nyanda za Malisho na Rasilimali za Vyakula vya Wanyama, Sheria ya Uhamiaji na Sheria ya Tasnia ya Nyama.

Pia kufanya marekebisho katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Idara ya Uhamiaji na Jeshi la Magereza, Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma na Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori.

Akiwasilisha bungeni jana maelezo ya muswada huo, Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Prof. Aderladus Kilangi, alisema muswada unapendekeza kurekebisha kifungu cha tisa cha Sheria ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu, ili kuanzisha kosa la kutoa taarifa binafsi za waathirika wa usafirishaji wa binadamu.

Alisema marekebisho hayo yanalenga kuzuia utoaji wa taarifa za waathrika kinyume cha sheria na kuhakikisha maisha binafsi na utambulisho wa waathirika unalindwa.

"Kifungu cha 10 kinarekebishwa, ili kuwezesha taarifa kuhusu makosa ya usafirishaji wa binadamu kutolewa na mtu yeyote badala ya mwathirika pekee.

"Marekebisho haya yana lengo la kutoa, kwa kila mtu jukumu la kutoa taarifa za utendaji wa makosa kwa mamlaka husika.

"Kifungu cha 12 kinarekebishwa, ili kumpa mtu yeyote anayemkamata mshukiwa wa usafirishaji wa binadamu jukumu la kumfikisha mtu huyo katika kituo cha polisi kilicho karibu," alisema.

Prof. Kilangi alisema kifungu cha sita (6) cha sheria hiyo kinarekebishwa, ili kuweka masharti kwa kesi zinazohusisha makosa makubwa ya usafirishaji wa binadamu kusikilizwa katika Mahakama Kuu.

Alisema kifungu kipya cha 8A kinapendekezwa kuongezwa, ili kuweka masharti yatakayozuia majaribio ya kutenda makosa ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema marekebisho haya yanalenga kuhakikisha majaribio ya kutenda makosa chini ya sheria hiyo, yanawekewa adhabu.

"Kifungu cha 26 kinarekebishwa, ili kutoa nafasi kwa mapato yanayotokana na mali zilizokamatwa au kutaifishwa katika utendaji wa makosa chini ya sheria hii kuweza kuwekwa katika Mfuko wa Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu.

"Kifungu cha 30 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kuondoa ukomo wa idadi ya watu wanaoweza kuteuliwa kuhudumu katika Sekretarieti ya Kamati ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu.

"Marekebisho haya yanalenga kumwezesha waziri kuamua na kuteua idadi ya watu watakaohudumu katika sekretarieti kulingana na wajibu na majukumu ya sekretarieti.

"Kifungu cha 31 kinapendekezwa kurekebishwa kwa kumwongeza mwakilishi kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika Kamati ya Kuzuia Usafirishaji wa Binadamu na kuainisha muda wa kushika madaraka kwa wajumbe wa kamati hiyo.

"Kifungu kipya cha 34A kinapendekezwa kuongezwa, ili kuweka adhabu ya jumla kwa makosa ambayo adhabu mahsusi haijaainishwa. Lengo la marekebisho haya ni kuhakikisha kuwa makosa yote chini ya sheria yanawekewa adhabu," alisema.

Prof. Kilangi pia alisema sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza marekebisho katika Sheria ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya, ili kuongeza uzito wa bangi na mirungi kwenye makosa yanayosikilizwa katika Mahakama Kuu au Mahakama za Wilaya.

Alisema Lengo la marekebisho hayo ni kupunguza mrundikano wa kesi mahakama za wilaya zinazosubiri kupelekwa Mahakama Kuu, kwa ajili ya kusikilizwa.

Akiwasilisha maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Katiba na Sheria kuhusu muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Najima Murtaza Giga, alisema kamati imekubaliana na hoja kesi za makosa makubwa ya usafirishaji wa binadamu zisikilizwe na Mahakama Kuu kutokana na suala hilo kuwa nyeti.

Najima pia alisema kamati inashauri serikali katika kubadili hadhi ya Idara ya Uhamiaji kuwa jeshi, ione haja ya kufanya marekebisho kwenye Ibara ya 147 ya Katiba ya nchi, ili kuijumuisha idara hiyo katika orodha ya majeshi nchini.

## Ng'ombe wa serikali kuhesabiwa rasmi

**Na Beatrice Shayo**

WAZIRI wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, ameagiza ng'ombe wote wa serikali kuingizwa kwenye mfumo wa utambuzi ili kusaidia kupata idadi ya mifugo nchini.

Waziri Ndaki aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati wa uzinduzi wa kiwanda cha kutengeneza hereni za kielekroniki za utambuzi wa mifugo nchini.

Alisema ng'ombe wa serikali katika maeneo mbalimbali wanatakiwa kuingizwa kwenye mfumo huo.

"Ni vizuri kuwa na mfumo mmoja utatusaidia kama nchi kwa kuwa tutatambulika kuwa tuna rasilimali za mifugo inayotoka Tanzania kiasi hiki... pamoja na ng'ombe wa serikali na wa watu binafsi tusiwe na utambulizi tofauti," alisema.

"Kuna baadhi ya watu wanatukodisha mashamba yetu wanasema wana ng'ombe kumbe hawana, tutajuaje hawana usajili, huu mfumo wa utambuzi utatusaidia kubaini mmiliki halali wa ng'ombe na wale wanaoiba mifugo."

Pia, Waziri Ndaki aliagiza ubadilishaji wa umiliki wa ng'ombe endapo mtu anataka kuuza mifugo yake ufanywe kwa haraka bila kuwapo na ucheleweshaji.

"Namna ya kubadilisha umiliki wa ng'ombe kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine unakuwa na mchakato mrefu kitu mbacho sisi wafugaji huwa hatupendi mara uende kwa mtendaji wa kijiji, mtendaji wa kata mara umtafute mtaalamu aweke taarifa kwenye kompyuta mara kompyuta ikosekane kijijini kunakuwa na mlolongo mrefu," alisema.

Alitoa wito kwa sekta binafsi kushiriki uwekezaji katika maeneo ya serikali hasa uzalishaji, mifugo na uvuvi ili kusaidia kuinua vipato vya wananchi.

"Sekta binafsi lazima muingilie kati ili kuongeza thamani ya mazao yetu ya mifugo watizame changamoto tulizonazo ili kutatua ni vizuri wakaiga mfano uliofanywa na hiki kiwanda," alisema.

Awali, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Hezron Nonga, alisema kuna maelekezo yalitolewa kwa ajili ya mifugo yote kutambuliwa na kusajiliwa.

Alisema mwaka 2017 walianza utambuzi kwa kupiga chapa jambo ambalo lililalamiwa kwa sababu chuma kilikuwa kinaunguza ngozi na kuonekana kwa alama.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu (katikati), akikata utepe jijini Dodoma jana, kuashiria kukabidhiwa pikipiki 75 zenye thamani ya Sh. milioni 118 kwa ajili ya makatibu wasaidizi wa Tume ya Utumishi wa walimu wa mikoa mbalimbali nchini. **PICHA IBRAHIM JOSEPH**

# Serikali kutoa tamko kuhusu 'tuition' shuleni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia zinatarajia kutoa tamko kuhusu masomo ya ziada 'tuition' kwa wanafunzi wa shule za msingi.

Aidha, imeagiza Tume ya Utumishi ya Walimu (TSC) kupitia upya na kusimamia adhabu zinazotolewa kwa walimu wanaokutwa na makosa ya kufanya mapenzi na wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Waziri wa TAMISEMI, Ummy Mwalimu, aliasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akikabidhi pikipiki 75 kwa Makatibu wa Wasaidizi wa TSC ngazi ya wilaya.

Alisema suala hilo baadhi ya walimu wamelifanya kama mradi jambo ambalo halikubaliki.

"Najua tuition inasaidia vijana kujiongeza kielimu, lakini baadhi yenu wanafanya kama mradi, unakuta watoto wa darasa la kwanza mpaka saa mbili yuko tuition sasa anapata muda wapi wa kupumzika, tutakutana TAMISEMI na Wizara ya Elimu ili kuona namna ya kuliweka sawa suala hilo na kulitolea tamko," alisema.

Akizungumzia walimu wanaojihusisha na mapenzi na wanafunzi, Waziri Ummy alisema adhabu zifanyiwe marekebisho ili kukomesha vitendo hivyo visijirudie.

Alisema walimu wanafanya makosa hayo na baadaye kurejeshwa kazini, suala ambalo linapaswa kuangaliwa kwa undani ili iwe fundisho kwa wengine.

Pia, Waziri Ummy alisema serikali haihitaji kuona walimu wa aina hiyo na kwamba Tume hiyo itawajibika kuhakikisha walimu hao wanapata adhabu stahiki kulingana na makosa wanayofanya.

Alisema TSC inapaswa kuangalia namna ya kufunga mfumo ambao utasaidia kujua mahudhurio ya walimu shuleni ili kupunguza utoro wa vipindi vya darasani.

Aliitaka Tume hiyo kuwafuatilia walimu 6,945 wa ajira mpya ili kuona kama wameripoti katika vituo vya kazi na kuingizwa katika mfumo.

"Kumezuka tabia ya walimu wanakwenda kuangalia vituo walivyopangiwa na baadaye wanaondoka vituoni hapo," alionya.

Akizungumzia upandaji ngazi, alisema asilimia 96 ya walimu hupandishwa madaraja na tayari wameanza kulipwa mishahara ya madaraja waliopandishwa.

Katika hatua nyingine, aliwaonya walimu wakuu wa shule mbalimbali kuhusu mialiko ya wageni rasmi wanaowaalika katika shule kuzingatia weledi wa mtu na maadili aliyokuwa nayo mbele ya jamii.

Kuhusu pikipiki zilizotolewa alisisitiza zitumike kwa ajili ya shughuli za serikali na sio kuzifanyia biashara ya bodaboda.

Kwa upande wake, Katibu wa TSC, Paulina Mkwama, alishukuru serikali kwa kulipa madeni ya walimu na kuwapandisha madaraja.

# RC Makalla kuvalia njuga maboresho mnada Pugu

**Na Maulid Mmbaga**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amesema atahakikisha anasimamia ipasavyo maboresho ya mnada wa Pugu na machinjio ili yaweze kuendana na hadhi ya jiji hilo baada ya kubaini kulega lega kwa suala hilo.

Aliyasema hayo jana jiji hapo baada ya kukutana na wadau wa sekta ya mifugo pamoja na Waziri Mashimba Ndaki, kujadili hali ya ubovu wa mnada huo, ambao mkandarasi anayeusimamia kuonekana kusuasua.

Alisema mazungumzo hayo yalikuwa na mafanikio makubwa baada ya Waziri Ndaki kumkabidhi jukumu la kumsimamia na kumbana mkandarasi amalize kazi ya kuboresha mnada huo baada ya kutoridhishwa na hali aliyoikuta wakati alipofanya ziara mnadani humo hivi karibuni.

Miongoni mwa changamoto zilizoonekana kuwapo katika mnada huo ni miundombinu mibovu inayohatarisha usalama wa mifugo pamoja na kasi isiyoridhisha ya mkandarasi aliyekabidhiwa kufanya marekebisho katika eneo hilo.

"Kwa sasa niahidi kuwa nitamsimamia ipasavyo mkandarasi ili kuhakikisha anakamilisha maboresho ya mnada kwa wakati na kupunguza changamoto zilizokuwa zikiwakabili wafugaji na wafanyabiashara katika eneo husika," alisema Makalla.

Pia, alisema endapo mnada huo utakuwa katika hali nzuri itasaidia pia machinjio ya kisasa ya Vingunguti kupokea mifugo yenye ubora utakaochochea upatikanaji wa nyama zenye ubora.

Miongoni mwa maboresho yanayotakiwa kufanyika katika mnada huo ni ujenzi wa uzio unaozunguka eneo husika, sakafu, eneo salama la kupakia ng'ombe, ujenzi wa vyoo na kero ya ukosefu wa maji. Mambo ambayo mkuu huyo aliahidi kusimamia mchakato wa utatuzi wake.




Mkuu wa Wilaya ya Nyang'hwale, mkoani Shinyanga, David Jamhuri (kushoto), akipokea msaada wa pikipiki nane kutoka kwa Mrakibu wa Idara ya Uhusiano ya mgodi wa dhahabu wa Barrick Bulynhulu, William Chungu, zilizotolewa na kampuni hiyo kwa ajili ya kuwezesha maofisa wa serikali wilayani humo kutembelea miradi ya kijamii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumiaji mawasiliano watahadharishwa

**Na Costantino Michael,** TUDARCo

WATUMIAJI wa huduma za mawasiliano wametakiwa kuhakikisha wanatumia njia sahihi zinazokubalika kisheria, ili kuepuka mkono wa sheria na kuipotosha jamii.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Huduma za Mawasiliano (TCRA CCC), Mary Msuya, alisema kwa sasa kumekuwa na ongezeko kubwa la matumizi, yasiyo sahihi ya huduma za mawasiliano hasa kwa vijana jambo ambalo limesababisha baraza kuona kuna umuhimu wa kuendelea kutoa elimu.

"Baraza ni chombo imara na cha kutegemewa katika kutetea haki na maslahi ya watumiaji wa huduma na bidhaa za mawasiliano pamoja na kuleta maelewano miongoni mwa wadau wa sekta ya mawasiliano," alisema na kuongeza;

"Tumeendelea kujenga mtandao imara wa kuhamasisha na kuelimisha watumiaji juu ya haki na wajibu ikiwa ni pamoja na kutengeneza mazingira mazuri ya kufanya mashauriano na wadau mbali mbali wa sekta ya mawasiliano."

Aidha, alisema baraza lina jukumu la kuchukua maoni ya watumiaji wa huduma za mawasiliano na kushauriana na watoa huduma na sekta husika lengo likiwa ni kuhakikisha watumiaji wanapata haki zao za msingi na huduma bora.

"Tumeona bado changamoto kwenye usambazaji wa taarifa kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Taarifa inaweza kutolewa kwenye ngazi flani ya uamuzi ambayo ni sahihi, kunatokea upotoshaji kiasi kwamba kilichokusudiwa kumfikia mtumiaji kinakuwa si kile kilichokusudiwa. Hii inaletwa na kukua kwa sekta ya mawasiliano," alisisitiza Msuya.

Kwa mujibu wa katibu huyo, baraza limejizatiti kutoa elimu kutokana na ukuaji wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) na kuongezeka kwa matumizi ya mitandao ya kijamii.

# RAS ataka TEHAMA udhibiti wa mapato

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Pwani, Mwanasha Tumbo, amesema endapo halmashauri zitajipanga upande wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), kudhibiti mianya ya upotevu wa mapato fedha zinazopatikana zitajikita kutekeleza miradi ya maendeleo.

Tumbo alisema hayo jana mjini hapa alipokuwa akizindua mpango wa awamu ya pili wa usimamizi wa fedha na ukusanyaji wa mapato kwa watumishi wa Halmashauri za Chalinze, Mkuranga na Mji Kibaha.

Mpango huo unasimamiwa na Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na unatekelezwa kwa ufadhili wa Serikali za Uswisi, Ujerumani kupitia shirika la maendeleo (GIZ) na Umoja wa Ulaya.

Tumbo alisema halmashauri kupitia vitengo vya TEHAMA zinatakiwa kuangalia kwa undani namna ya kuondoa mianya ya upotevu wa mapato kwa kuwa yakikusanywa kwa wingi miradi mingi itatekelezwa.

"Tutahakikisha Pwani tunakuwa na mipango ya kuinua ukusanyaji wa mapato na kuyaweka kwenye matumizi bora, ili tuendane na mradi huu, ambao umelenga kuondoa vikwazo kwenye ukusanyaji wa mapato," alisema.

Alisema katika halmshauri za mkoa huo katika ukusanyaji wa mapato umefikia zaidi ya asilimia 80 huku Chalinze ikiwa kinara kwa kufikia asilimia 100 na kupitia mradi huo zitafanya vizuri zaidi.

Katibu tawala huyo alisema mapato yakikua, migogoro kwenye jamii itapungua na wananchi watajikita kwenye shughuli za kiuchumi.

Aliongeza kuwa mtumishi yeyote atakayebainika. kuhusika kwenye upotevu wa mapato hatua zitachukuliwa

Mtaalamu mshauri wa mradi wa Usimamizi wa fedha na kusanyaji wa mapato kutoka GIZ, Raymond Nzali, alisema mradi huo unatekelezwa nchini katika halmashauri 21 kwa ufadhili wa Uswisi, Ujerumani na Umoja wa Ulaya.

Alisema wameona kuna haja ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwenye halmashauri na wamejipanga kujenga uwezo upande wa TEHAMA na kuwekeza huko kuziba mianya ya upotevu wa mapato.

Nzali alisema katika Mkoa wa Pwani utafanya kazi na halmashauri na usimamizi utafanywa kwenye ngazi ya mkoa.

HABARI KITAIFA

## CMS yaongezea ujuzi uchimbaji wataalamu

**Na Christina Mwakangale**

KAMPUNI ya uchimbani madini ya CMS imewaongezea ujuzi wataalamu wake wa uchimbaji kwa kuwapa mafunzo ili kukidhi matumizi ya mfumo mpya katika kuchimba madini kielektroniki.

Mwenyekiti wa CMS Tanzania Limited, Balozi Ami Mpungwe, akizungumza hivi karibuni kuhusu uwekezaji wa mitambo mipya ya kielektroniki, alisema teknolojia hiyo ni ya kipekee kwenye uchimbaji wa chini ya ardhi barani Afrika.

Alisema kutokana na hilo timu maalum za uchimbaji na ufundi zimeandaliwa kwa ajili ya kutumia mifumo ya hali ya juu ya umeme ili kuongeza ufanisi zaidi kwenye utendaji kazi na hali ya usalama.

"Tunaimani na sekta ya madini nchini Tanzania kama iliyoweza kuonyeshwa kupitia jitihada endelevu za kujitoa kwetu kikamilifu kwa zaidi ya miaka 16. Kwa jinsi hii, tunaendelea kujizatiti katika kutoa teknolojia bora na yenye viwango kwa wateja wetu waliopo hapa.

"Uwekezaji mkubwa uliofanywa kwa ajili ya mtambo huu pamoja na mpango wa ujio wa mitambo mingine miwili nchini, mwaka huu, mtambo mmoja tayari upo njiani kuelekea kwenye mgodi wa dhahabu wa Bulyanhulu."

Alisema tayari CMS imewekeza zaidi ya shilingi bilioni nane, kwenye mitambo ya Swick Gen II Mobile Drill kuunga mkono sekta ya madini nchini, imenunuliwa kwa ajili ya kuongeza ubora uchakataji wa madini, kuendeleza huduma za uchimbaji kwa kampuni ya Barrick kwenye mgodi wa Bulyanhulu.

"Mitambo hiyo mipya ni ya kwanza kuwahi kutumika barani Afrika, yenye uwezo mkubwa na teknolojia ya kipekee kwa ajili ya shughuli za madini pamoja na mifumo unayohakikisha usalama wa wafanyakazi wa uchimbaji katika kiwango cha hali ya juu."

Pia, Mpungwe aliongeza kwamba kampuni imeanzisha vituo vipya mkoani Mwanza kwa ajili ya utekelezaji wa operesheni mbalimbali nchini vya kutengeneza na kuunda vifaa vingine huku ikiajiri Watanzania 418, wanaofanya kazi idara mbalimbali za biashara za kampuni hiyo.

# Faini sasa mil.1/- kuharibu miundombinu kuzimia moto

**Na Sanula Athanas,**
DODOMA

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji wa Mwaka 2021, ambao pamoja na mambo mengine, inaongeza adhabu kwa wanaoharibu miundombinu ya kuzimia moto (fire hydrants).

Kwa mujibu wa muswada huo, adhabu sasa inaongezwa kutoka faini isiyozidi Sh. 200,000 hadi kufikia faini isiyopungua Sh. 500,000 na isiyozidi Sh. milioni moja.

Muswada huo ulisomwa kwa mara ya kwanza Bungeni Agosti 31, mwaka huu, ukiwasilishwa kwa hati ya dharura.

Akiwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu muswada huo, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Mussa Zungu, alisema bungeni jijini Dodoma juzi jioni kuwa kamati imejiridhisha adhabu hiyo itasaidia kuwafanya wananchi kutambua umuhimu wa kuilinda miundombinu ya kuzimia moto.

"Vilevile, kamati inaona kuwa adhabu hii inalingana na madhara ambayo yanasababishwa na kushindwa kuzima moto kutokana na uharibifu uliofanywa na watu. Hii itasaidia kuhakikisha udhibiti wa majanga ya moto kupatikana kwa urahisi.

"Hata hivyo, kwa kuwa miundombinu mingi imeshaharibiwa kwa kujua au kutokujua, kamati imesisitiza kuwa adhabu inayopendekezwa na marekebisho ya sheria hii isiziguse taasisi au wananchi walioharibu miundombinu hiyo kabla ya sheria hii kupitishwa," alisema.

Zungu pia alisema kamati yao ilijiridhisha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ni miongoni mwa majeshi yaliyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya nchi na kwa kuzingatia vikwazo vilivyojitokeza katika utekelezaji wa majukumu ya jeshi hilo ikiwamo askari kujeruhiwa, wizi na uharibifu wa miundombinu, marekebisho hayo ya sheria kuwawezesha askari wake kutumia silaha, ni muhimu.

"Hii itawezesha Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kuimarisha usalama wa miundombinu yake ikiwa ni pamoja na ofisi na magari ya Zimamoto, usalama wa maofisa na askari hususan wakati wa matukio ya moto, kuzuia wizi kwenye majengo na maeneo ambayo yamekutwa na matukio ya moto. Vilevile, kuliwezesha jeshi kutumia silaha hizo katika mafunzo," alisema.

Aliongeza kuwa kamati pia ilijiridhisha kuwa uzoefu wa kumiliki silaha upo katika Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Tanzania Zanzibar na vilevile katika nchi za Afrika za Algeria, Misri, Morocco na Msumbiji.

Mbali na madhumuni tajwa hapo juu, muswada huo pia unapendekeza kuweka masharti kwa wamiliki wa majengo yanayozidi mita 12 kutoka usawa wa ardhi, kuwasilisha michoro ya majengo yao Jeshi la Zimamoto na Uokoaji ili kupewa ushauri wa kudhibiti majanga ya moto.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, wakati wa mjadala kuhusu muswada huo, aliahidi wizara itahakikisha hakutakuwa na urasimu ndani ya Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika kushughulikia vibali vya ujenzi wa majengo yenye sifa hizo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa (kulia), akipata maelezo kutoka kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba (kushoto), wakati wa uzinduzi wa Mfumo wa Pamoja wa Utoaji Huduma kwa Taasisi za Umma unaoratibiwa na Shirika la Posta nchini. Uzinduzi huo ulifanywa jana jijini Dar es Salaam. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NMB Foundation yaja na uwekezaji kwenye sekta 5

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NMB imezindua asasi ya kiraia iitwayo NMB Foundation, inayolenga kujikita katika kuimarisha uwekezaji wake kwa jamii katika sekta tano teule.

Hatua hiyo inakwenda sambamba na Mpango Maalum wa Udhamini wa Masomo 'NMB Nuru Yangu Scholarship and Mentorship,' ambapo uzinduzi uliohudhuriwa na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Kupitia NMB Foundation, benki hiyo inaunga mkono zaidi jitihada za serikali kuimarisha maendeleo, ambako inaenda kuvuka mipaka ya Programu ya Uwajibikaji kwa Jamii, ambayo kwa miaka 16 ya uwepo wake, imetumia zaidi ya Sh. bilioni 12 za urejeshaji kwa jamii kupitia asilimia moja ya faida yake kila mwaka.

Akizungumza wakati wa uzinduzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa NMB, Ruth Zaipuna, alisema asasi hiyo imejipanga kuacha alama kwa jamii ya Kitanzania, kupitia uwekezaji na urejeshaji kwa jamii (CSR) kwenye sekta tano za kipaumbele ambazo ni elimu, afya, kilimo, mazingira na ujasiriamali.

Akichanganua majukumu ya NMB Foundation, Zaipuna alisema katika elimu wanatarajia kutoa misaada zaidi ya ilivyokuwa ikifanya kupitia CSR, ambako itajielekeza kukuza elimu na kuongeza idadi ya watoto wanaopata elimu, huku kwenye afya ikilenga kuboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa makundi maalum na jamii kwa ujumla.

"Kwa upande wa mazingira, tunakusudia kuhamasisha utunzaji wake kwa lengo la kuboresha makazi ya jamii, wakati kwenye kilimo nia ni kuimarisha uwezo wa vyama vya ushirika na kuwaongezea ujuzi kupitia elimu na mafunzo ya masuala ya fedha, biashara na kuwajengea wakulima uwezo wa kukopesheka.

"Katika ujasiriamali, NMB Foundation itahakikisha inafanikisha juhudi za uzalishaji na utoaji ajira, lakini kukuza uchumi kwa kutoa mafunzo na uwezeshaji wa elimu ya fedha, matumizi ya dijitali, ubunifu na uendelezaji wa biashara ili kuharakisha mabadiliko chanya katika sekta hiyo, inayokusanya kundi kubwa la vijana," alisisitiza Zaipuna.

Kupitia 'NMB Nuru Yangu Scholarship and Mentorship,' Zaipuna alifafanua kuwa ni programu ya ufadhili wa masomo kwa vijana wa ngazi ya chuo na sekondari wanaotoka katika familia zisizojiweza, ambao utaanzia mwaka huu wa masomo wa 2021/22, wanakoratarajia kusaidia vijana 200, wakiwamo wanachuo wa shahada ya kwanza 50 na wanafunzi wa sekondari 150 kote nchini.

Kabla ya kuzindua NMB Foundation na NMB Nuru Yangu Scholarship, Majaliwa aliipongeza NMB kwa ubunifu uliozaa asasi na programu zilizozinduliwa, ambazo ni rafiki kwa jamii, zinazoenda moja kwa moja kusapoti jitihada za serikali katika kusimamia maeneo yote yaliyotajwa katika vipaumbele vitano vilivyoainishwa.

Alibainisha kuwa, NMB sio wageni wa kuunga mkono jitihada za serikali kutatua changamoto za kijamii na kwamba NMB Foundation na NMB Nuru Yangu, ni kielelezo cha benki inavyojitoa katika kuitendea haki jamii ya Watanzania na kuwa kupitia CSR, kwa miaka mitano iliyopita benki hiyo imeweza kuwafikia wanufaika zaidi ya milioni tano kote nchini.

"Uzinduzi huu una baraka zote za serikali, kwa sababu tunatambua kuwa asasi hii ni muhimu kwa ustawi na maendeleo ya Taifa na watu wake, kama ilivyo pia kwa Programu ya NMB Nuru Yangu, ambayo inaenda kuwabeba mamia ya vijana wetu kutoka katika jamii ya wasiojiweza, ambao sisi kama Serikali tayari tumeshawekeza vya kutosha katika kuwakomboa kielimu.

"Serikali tunaahidi sapoti ya kila namna kwa NMB kutokana na jinsi inavyojitoa katika kutuunga mkono kwenye maeneo mbalimbali," alisema Majaliwa.

# Utekelezaji uamuzi wa migogoro waandaliwa

SERIKALI imeandaa mpango kazi kwa ajili ya kuwaeleza wananchi juu ya uamuzi wake kuhusu migogoro kati ya wananchi na hifadhi, ikiwa ni utekelezaji wa uamuzi wa Baraza la Mawaziri.

Wizara ya Maliasili na Utalii ilibainisha hayo jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Kondoa (CCM), Dk. Ashatu Kijaji.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali lini itaelekeza kwa wananchi uamuzi wa timu ya mawaziri iliyozunguka kwenye maeneo yenye migogoro kati ya wananchi na mapori ya hifadhi.

"Je, ni lini serikali kwa kushirikiana na wananchi itaweka mipaka kati ya mapori ya hifadhi na vijiji vinavyozunguka ili kupunguza migogoro iliyopo na kuwezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi bila usumbufu?" Alihoji.

Wizara ilisema katika majibu yake kwamba katika kutekeleza mpango kazi huo, timu ya mawaziri wa kisekta itapita katika mikoa husika kwa lengo la kutoa elimu na ufafanuzi kwa viongozi wa mikoa na wilaya.

Ilisema kazi hiyo itakwenda sambamba na timu ya wataalam itakayojumuisha Ofisi ya Rais Tawala za Mikao na Serikali za Mitaa, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, uongozi wa mikoa, wilaya na vijiji.

Aidha, ilisema kazi ya uwekaji wa mipaka kwenye maeneo yote yenye migogoro itafanywa na timu ya wataalamu kutoka katika sekta za Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na Wizara ya Maliasili na Utalii.

Ilibainisha timu hiyo itapita katika maeneo yote ili kufanya tathmini, uhakiki na kuweka mipaka kulingana na uamuzi wa serikali.

Kadhalika, ilisema wananchi watashirikishwa ili kuondoa uwezekano wa kujitokeza migogoro mingine.



Mbunge wa Jimbo la Mwera, Zahor Mohamed Haji, akichangia hoja jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

## Ataka kinamama kulindwa na zebaki

MBUNGE wa Viti Maalum (CCM), Kabula Shitobelo, ameitaka serikali kuwakinga kinamama wanaochenjua dhahabu na sumu ya zebaki kwa kuwa ina madhara makubwa kiafya.

Akiuliza swali bungeni jana, Shitobelo alihoji serikali ina mpango gani wa kuwakinga kinamama hao.

Katika majibu ya Wizara ya Madini, ilisema mpango wa serikali katika kuwakinga kinamama wanaochenjua dhahabu kwa kutumia kemikali ya zebaki ni kuendelea kutoa elimu ya uchimbaji na uchenjuaji salama wa madini pamoja na madhara ya kemikali hiyo kwa wachimbaji wadogo.


Ilisema elimu hiyo inatolewa na Wizara ya Madini kupitia Tume ya Madini, Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania (GST), Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC).

Pia ilisema katika utekelezaji wa mpango huo, serikali kupitia Wizara ya Madini imejenga vituo vitatu vya mfano vya uchenjuaji wa madini ya dhahabu katika maeneo ya Itumbi (Chunya), Lwamgasa (Geita) na Katente (Bukombe) ambayo yameonekana kuwa na wachimbaji wadogo wengi zaidi.

Ilibainisha kuwa teknolojia ya uchenjuaji inayotumika katika vituo hivyo ni Carbon –in –Pulp (CIP) ikiwa ni mbadala wa matumizi ya kemikali ya zebaki.

Hata hivyo, ilisema zipo kampuni za uchimbaji mdogo ambazo zimeanza kuchenjua dhahabu kwa kutumia teknolojia ya 'shaking table' ambayo haitumii zebaki wala kemikali yoyote.

Ilisema teknolojia hiyo wizara inaendelea kuifanyia majaribio ili kuona tija yake kabla ya kuanza kuitumia kwa wachimbaji wote hasa wadogo.




# Matumbawe bandia yawekwa kurejesha mazalia ya samaki

BUNGE limeelezwa kuwa serikali imeanza kuweka matumbawe bandia katika maeneo kadhaa ya mwambao wa Bahari ya Hindi hususan Dar es Salaam, Unguja na Pemba ili kurejesha mazalia na makulia ya samaki yaliyoharibika.

Ofisi ya Makamu wa Rais, Muungano na Mazingira, iliyasema jana bungeni ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Wingwi (CCM), Omar Issa Kombo.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji lini serikali itaweka matumbawe bandia na kupanda mikoko katika bahari ili kurejesha mazalia hayo.

Kwa mujibu wa ofisi hiyo, eneo la Sinda pwani ya Dar es Salaam lenye mita za mraba 2,000 limepandikizwa matumbawe bandia.

Vilevile, ilisema kwa upande wa Unguja na Pemba, matumbawe bandia 90 aina ya 'reef ball' yalipandikizwa katika kijiji cha Jambiani na matumbawe bandia 46 na mapande maalum sita katika kijiji cha Kukuu.

Pia ilisema matumbawe hayo yalifuatiliwa ukuaji wake kitaalam na matokeo yameonyesha mafanikio makubwa kwa kuimarika kwa mazalia ya samaki, hivyo kuongezeka kwa kiwango cha samaki katika maeneo hayo.

Wizara pia ilisema serikali imekuwa ikiongeza jitihada zaidi katika upandaji wa mikoko kwenye fukwe mbalimbali za nchi nzima kwa kushirikiana na asasi binafsi na washirika wa maendeleo.

Ilifafanua kuwa takribani hekta saba za mikoko zilipandwa Unguja na hekta 10 zilipandwa Pemba kwa mwaka 2020/21.

Kadhalika, ilisema upandaji wa hekta 13.5 unaendelea mpaka sasa na matarajio ni kupanda hekta 15 kwa mwaka huu.

Aidha, ilisema kwa upande wa Tanzania Bara, hekta 105 zimepandwa katika Delta ya Rufiji na matarajio ni kupanda hekta 2,000 kwa pwani yote ya Tanzania Bara ifikapo mwishoni mwa mwaka 2022.

Pia ilisema ni wajibu wa wananchi kuhakikisha wanatunza, kuhifadhi na kusimamia matumbawe na mikoko, pamoja na mifumo ikolojia inayopatikana ndani ya bahari.

## Aliyemrithi Maalim Seif atoa msimamo wa ACT na katiba



Ukurasa 12



Ukurasa 14

## HIBATULLAH AKHUNDZADA Kiongozi mpya Afghanistan aliyejitokeza kwa kishindo kusimamia dini na serikali



# Mtazamo mtambuka ujio mkutano wa Msajili, IGP na vyama vya siasa

**Na Sabato Kasika**

KATIKA juhudi la kutaka kumaliza kile kinachoonekana kwamba upo uhasama kati ya Jeshi la Polisi na vyama vya siasa, Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa inatarajia kukutanisha makundi hayo kwenye kikao maalum.

Ingawa tarehe rasmi ya kikao hicho haijatangazwa, lakini ofisi hiyo inatarajia kukutanisha makundi hayo mawili, kuweka sawa utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa bila kukwaruzana.

Msajili wa vyama hivyo, Jaji Francis Mutungi, amesema juzi kuwa, wakati wanasubiri kufanyika kikao hicho, hatarajii kuona vyama vya siasa vikiandaa kufanya mikutano na makongamano kabla ya mkutano huo.

Jaji Mutungi ambaye kwa wadhifa wake, ndiye mlezi wa vyama na msimamizi wa kisheria, anasema mvutano kati ya vyama hivyo na Polisi, unaweka taswira hasi kwa umma.

Kutokana na uamuzi huo, baadhi ya wadau waliozungumza na gazeti hilo, wametoa maoni yao na jinsi wanavyochukulia hatua hiyo ya Msajili



Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Francis Mutungi. **PICHA: MTANDAO**

### AMECHELEWA SANA

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha Wananchi (CUF), Magdalena Sakaya, anasema Msajili amechelewa kuchukua hatua hizo na kufafanua kuwa, ni miaka mitano sasa tangu Polisi ianze utaratibu wa kujitokeza kwenye mikutano ya vyama vya siasa.

"Hatua za Msajili wa Vyama vya Siasa ya kutaka kukutana na Jeshi la Polisi na viongozi wa vyama vya siasa ni nzuri. Lakini, ninasikitika kwani mambo anayotaka kuzungumzia yamekuwapo kwa miaka mitano," anasema Sakaya.

Anafafanua kuwa, Msajili akiwa ni mlezi wa vyama vya siasa, anapaswa kukemea hali hiyo, tangu mwanzo na vyama viwe huru kufanya shughuli zakena kwamba ukimya umezua sintofahamu iliyopo sasa.

"Zuio la mikutano ya siasa halipo kisheria bali ni tamko la mtu ambalo limeendelea kutumika huku msajili akiwa kimya. Sisi vyama vya siasa, tumeumizwa sana na tamko hilo," anasema.

Anafafanua kuwa, CUF ni miongoni mwa vyama vilivyoonja anachokiita 'kamatakamata ya polisi' hata kwenye vikao vya ndani na ufunguzi wa matawi sehemu mbalimbali nchini.

"Inauma sana kuona vyama vya upinzani vikizuiwa kufanya mikutano huku CCM ikiwa huru na kama kweli Msajili amedhamiria kwa dhati kumaliza kero hii aruhusu sheria ifanye kazi, hasa ile ya vyama vya siasa ya Mwaka 1992 ambayo inaruhusu vyama kufanya mikutano ya hadhara," anasema.

### POLISI IELEKEZWE

Mchambuzi wa siasa, Gwandumi Mwakatobe, anashauri ni vyema kama Msajili angekuwa na utaratibu wa kufanya mikutano hiyo kila mara na kwamba, utaratibu utapunguza sintofahamu iliyopo sasa.

"Kama angekuwa na mikutano hiyo mara kwa mara kati yake na wadau hao, kila upande ungetimiza wajibu bila kugombana. Lakini alikuwa kimya kwa zaidi ya miaka minne wakati hayo yakitokea," anasema.

Mwakatobe anaeleza binafsi inamshangaza kuona polisi wanaotakiwa kuzuia vurugu kwenye mikutano ya siasa anayoitaja nu fursa yao kisheria, waisambaratishe, sambamba pamoja ma hatia kadhaa.

"Sheria na Katiba ya nchi vinaruhusu mikutano ya vyama vya siasa, hivyo kile ambacho anaitisha kati yake na polisi na wanasiasa kwa ajili ya majadiliano, hakina nguvu zaidi ya sheria na Katiba," anasema.

Mchambuzi huyo anafafanua kuwa, Msajili anatakiwa kuwaleleza polisi kufuata sheria na Katiba, ili vyama vya siasa viendelee na shughuli zake kama kawaida, kwa kuwa vipo kisheria na kikatiba.

### NI MWANZO NZURI

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba Tanzania (JUKATA), Bob Wangwe, anasema hatua anazochukua Msajili wa Vyama vya Siasa, ni mwanzo mzuri ambao huenda ukavifanya vyama vya kuendelea na mikutano ya siasa kwa uhuru.

"Kwa kawaida meza ya majadiliano huwa inaleta muafaka. Hivyo, ninaamini kwamba huo ni mwanzo mzuri ambao unakwenda kufungua ukurasa mpya na kuondoa utata, ambao umekuwapo kwa miaka mitano," anasema Wangwe.

Kwa mujibu wa Wangwe, Sheria Namba Tano ya Vyama vya Siasa iliyofanyiwa marekebisho Mwaka 1999, inaviruhusu vyama kuendesha mikutano bila kizuizi na kwamba, anaamini mkutano huo utaliweka jambo hilo sawa.

"Binafsi ninaamini kwamba, mabadiliko ya uongozi wa kiasi yaliyofanyika hivi karibuni, yanaweza kuwa na mchango mkubwa kwenye utata huo ambao umeleta msuguano kati ya wanasiasa na polisi," anasema.

### MWELEKEO WA MSAJILI

Msajili anasema, lengo la mkutano huo ni kujadili namna ya kuondoa kile kinachoonekana kuwa upo uhasama kati ya Jeshi la Polisi na vyama vya siasa na namna ya kuweka vizuri utaratibu wa kuendesha mikutano ya kisiasa.

"Tunatarajia kufanya mkutano wa kuondosha mvutano unaojitokeza kati ya polisi na vyama vya siasa, yawezekana umma ukafikiri tumekalia kimya hilo suala, nikaona ni busara kuuhabarisha kwamba hatujakalia kimya hii hali ambayo inaonekana kama inaleta taharuki fulani," Jaji Mutungi anasema.

Anafafanua kuwa mvutano kati ya vyama hivyo na Jeshi la Polisi umeanza kujenga taswira hasi kwa umma na kwamba asingependa kuona watu waogopa, kila mkutano wa siasa, polisi wamejaa, kila shughuli ya wanasiasa polisi wanajaa.

"Sisi kama Ofisi ya Msajili, tunawiwa kuutarifu umma kuwa siasa ya nchi yetu haijafikia hatua hiyo ya taharuki zisizo na mbele wala nyuma, nisingependa kutumia neno ambalo wengi wamezoea kulitumia, sintofahamu. Sisi tunasema hakuna sintofahamu, ni suala tu la kuwekana wazi na kueleweshana."

# Aliyemrithi Maalim Seif atoa msimamo wa ACT na katiba

## •Aja na angalizo la kinamama nchini

**Na Waandishi Wetu**

KIFO cha Maalim Seif Shariff Hamad, kimemuibua Dorothy Semu, ambaye amechukua nafasi ya Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha ACT- Wazalendo, iliyokuwa ikishikiliwa na mkongwe huyo wa siasa za Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.

Katika mazungmzo yake na gazeti hili, jijini Dar es Saalam hivi klaribuni, pamoja na kushika nafasi hiyo anatamka "pengo la kiongozi huyo halizibika ndani ya chama."

Anamtaja Maalim Seif Shariff Hamad, alikuwa mfano mzuri katika kukuza na kulea viongozi wengine na kuwafanua wawe na msimamo usiyoyumba, kama kilivyoonyeshwa kwenye tozo za miamala ya simu na katiba mpya. Fuatilia mazungumzo ya ana kwa ana:

**SWALI:** Kwa wasiomfahamu Dorothy ni nani na historia yako ni ipi katika siasa?

**JIBU:** Mimi ni mama wa watoto watatu nimezaliwa Kilimanjaro. Kitaaluma ni mtaalamu wa Jiografia na nimelelewa na wazazi waliokuwa watumishi wa serikali.

Mimi ni Makamu Mwenyekiti wa ACT-Wazalendo Bara na nakaimu cheo cha Mwenyekiti Taifa, baada ya Maalim Seif, kufariki.

**SWALI:** Unajigawaje kutekeleza majukumu ya kichama na ya mama wa familia?

**JIBU:** Siasa ni tasnia ambayo inahitaji sana muda wako na ni maisha ya kila siku na inatuathiri katika kila nyanja.

Kwa hiyo, siasa zikiwa nzuri na maisha yetu yatakuwa bora. Kama mama, ninasema siasa inahitaji muda wako, inahitaji pia akili kwa kuwa mwanamke pamoja na kuwa unatakiwa uwe kiunganishi na mratibu wa mambo mengi.

Ninachoweza kusema huwa sijitahidi kuwa 'super woman', yaani kuwa ninapika mwenyewe, ninafua mwenyewe lakini ninajitahidi kuwa mratibu mzuri wa yale mambo yote niayotakiwa kuyafanya.

Ninatakiwa kuwa mama, hivyo ninafanya kazi yangu ya mama nyumbani lakini pale ambapo ninaona ninahitaji msaada au msaidizi, sijinyimi hiyo nafasi, ninajitahidi kuwa na wasaidizi sahihi mahali sahihi.

Na watu wanaonisaidia kazi, sio kwamba nimewaachia majukumu lakini kuwapo na ule usaidizi ni muhimu kwa sababu huwezi kubeba kila kitu kwa wakati mmoja, lazima yatakushinda au utaelemewa upande mmoja.

Ili uwe mratibu mzuri unahitaji uwe na wasaidizi wazuri, mume wangu ni msaidizi mkubwa kwenye ulezi, kwa hiyo, familia inaenda vizuri.

Ninajitahidi kuwa na watu watakaonisaidia vizuri kwenye siasa kuangalia majukumu yangu ni yapi, kuratibu wale walio chini yangu na kuhakikisha yote yanayotakiwa kufanyika yanafanywa kwa wakati.

Dhana ya kwamba mwanamke unatakiwa uwe 'super woman', ni kweli unakuwa mwanamke wa shoka lakini lengo sio kubeba kila kitu kwa pamoja kikakulemea. Badala yake ni kuvipangilia na kuratibu ili vyote vifanyike kwa wakati na ufanikiwe.

Tunawaambia wanawake tuwe wapangiliaji wa mambo, tuyaratibu yaende na wewe majukumu yako muhimu yawe yanakwenda vizuri na tusione ni udhaifu kwa mwanamke kuhitaji wasaidizi. Mwanamke unatakiwa upate wasaidizi bora zaidi ili kazi zako zifanikiwe zaidi.

**SWALI:** Kufariki Maalim Seif kumekiathiri vipi chama?

**JIBU:** Maalim Seif alikuwa ni gwiji na kungwi wa siasa. Ni mtu ambaye sidhani kama nina maneno ya kumwelezea. Nilipata nafasi ya kufanya naye kazi kwa miaka hii miwili na katika uenyekiti wake, alikuwa mfano katika kukuza na kulea viongozi wengine.

Kwa hiyo, kama taasisi tunaweza kusema tumefaidika na uwapo wa Maalim Seif kwa sababu amezaa watu wengine wengi imara na makini katika ujenzi wa chama chetu.

Tunapungukiwa kumkosa kama sehemu yetu, hekima, busara na ualimu wake, tumepungukiwa sana katika hilo na tunaamini ni pengo ambalo haliwezi kuzibika.

Lakini wakati huo huo tumepata faida kubwa, kuwa naye na kutufundisha, kutulea na kutuongoza vyema ili kesho na keshokutwa chama kiendelee kukua, kuwa imara na kinachotekeleza majukumu yake ya kimsingi.

Kwa hiyo, ninaweza kusema Maalim ameacha watu wengi ambao wanafanya kazi kwa umakini .

Mpaka leo unavyokiona, hakijakutana na changamoto tukashindwa kuitatua kwa umakini, kwa uwezo wetu kwa kufuata taratibu za chama kwa kushauriana na siku zote tunapopitia changamoto, sisi tunaona kama ni fursa ya kuwa bora zaidi.

**SWALI:** Ni ipi kauli yako kwa wanawake wanaofikiria kuingia kwenye ulingo wa siasa?

**JIBU:** Wanawake tunatakiwa tuondokane na dhana ya kuona kuwa siasa sio jambo letu. Hii ni hali inayoonyesha kwenye siasa ndipo kwenye nguvu kwa sababu tunaona maraisi wote wanachaguliwa na wanasiasa, ndiyo inayompa mtu nguvu ya kushika dola.

Kwa hiyo, huku tumeaminishwa kwamba hii sehemu ya nguvu sio sehemu ya wanawake, lakini sasa tunaona tuna Raisi mwanamke na tumebaini kuwa nguvu ya siasa pia ni sehemu ya wanawake.

Wanawake kwa sasa tunafikia zaidi ya asilimia 51 ya wanaopiga kura, sawa na ilivyo kwa idadi ya watu nchini. Hivyo, inatupa nguvu kwenda na wagombea ambao tunajua watajibu changamoto zetu za kila siku.

Hapo tunakuwa na wagombea ambao wataongelea maendeleo ya wanawake na wataleta mabadiliko kwa wanawake.

Kwa hiyo, mwisho wa siku wanawake tunakuwa na kura ya turufu katika siasa hasa kwenye kuchagua nani awe nani.

Kwa hiyo, kama mwanamke anapenda au anaona anashawishika kuingia kwenye siasa, kwanza ninamshauri ajiandae kisaikolojia hapa ni ushindani.

'Kuna ushindani achukulie kama ushindani chanya, siyo kama ni ugomvi. Kwa hiyo, akikutana na ushindani katika siasa ajue ni sehemu ya ushindani.

Na pili, kama jamii ya Kiafrika bado kuna mfumo dume, kwa hiyo, mwanamke asitegemee kwamba atakuta ametandikiwa zulia jekundu apite, bado atakutana na zile nguvu za watu wengine ambao watamuona hujawa tayari, hawezi kufanya hivi au vile.

Anachotakiwa kama mwanamke ni kujijua ni nani, kufanya kazi kwa bidii na kufahamu uwanja ambao umeamua kujikita unafanya nini ili uwe bora, uwe tayari kujifunza na kukosolewa.

Aidha kuwa tayari kunyumbulika kutokana na mazingira, na pia kujua ili uwe kiongozi bora, unatakiwa kufanya nini, ili uwe mwenyekiti bora wa kata unatakiwa kufanya nini, na kwenye siasa kuna kukosolewa, hivyo uwe tayari kukosolewa, kusikiliza, kujiangalia kufahamu kitu gani utafanya ili uwe bora zaidi kama kiongozi na ukumbuke kila wakati kwamba haya ni mashindano.



Dorothy Semu (kushoto ) katika harakati za kumnadi mgombea wa ACT- Wazalendo wakati wa kampeni za kisiasa, kisiwani Pemba. **PICHA: MTANDAO**

Kwa hiyo siyo kila muda mtu atakuachia upite kirahisi, wanawake mara nyingi wanasema eeh mwanamke mwenzangu ameniwekea pingamizi, ndio wana haki ya kukuwekea pingamizi. Kwa hiyo, ni kazi yako kujua kama mgombea ubunge, una haki ya kuwekea mgombea pingamizi, hawa wana vitu gani ambavyo unatakiwa kuwekea pingamizi.

Kwa kutambulia hilo, amka asubuhi kaweke pingamizi, usichukulie hasi kwamba anataka kukuangusha, ipokee kwa mtizamo chanya kwamba upo kwenye ushindani na unatakiwa upite mbele nishinde, nifanye jitihada zote chanya ushinde, ujinadi kwa usahihi, ujue eneo lako unalolifanyia kazi kama ni mgombea au ni kwenye uongozi wa chama.

Ufahamu ni mambo gani unatakiwa ufanye ili ushinde na ili uonekane bora zaidi ya wengine?

Changamoto zipo nyingi kutokana na mifumo ya maisha, hivyo utakutana na vitu ambavyo sio chanya kwako. Unatakiwa kuwa na uwezo wa kujua lipi la kufanya na la kuacha ili ufanikishe jambo lako na mwisho ulinda heshima yako na kujiheshimu.

Vyama vingi, hasa katika ACT-Wazalendo, vimeweka mifumo ambayo inawalinda wanawake ambao kama unaona unanyanyaswa au unafanyiwa kitu ambacho ni kinyume, una haki ya kwenda kusema na kusikilizwa katika kamati ya maadili.

**SWALI:** ACT-Wazalendo inaonekana kuwa na nguvu zaidi upande wa Zanzibar kuliko Bara. Mikakati yenu ni ipi katika kuimarisha chama Bara?

**JIBU:** Kwanza; ninaweza kusema siasa za Bara na Zanzibar ni tofauti. Mwamko wa kisiasa wa Wazanzibari upo tofauti na huu wa Bara.

Pili, siasa za Zanzibar zipo katika makundi mawili makubwa ACT upande mmoja na CCM upande mwingine lakini pia vyama vingine vipo ila haviwezi kufikia wingi kama wa viwili hivi.

Upande wa Tanzania Bara kuna vyama vingi lakini bado ACT tupo imara sana na sisi kwa kutambua hilo, unajua chama kinapitia awamu nyingi za kukua.

Tupo imara kwa sababu tumeweza kuweka wagombea katika uchaguzi wa serikali za mitaa, ubunge na pia tuna wawakilishi wanne bungeni.

Hata hivyo, sisi huku ni chama imara, chenye nguvu na ni wafuasi wengi. Lakini pia kwa upande wa Bara tumepata uzoefu.

Hapa Tanzania Bara kikao cha Kamati Kuu ya chama kinapigwa stop (kinazuiwa), tumeona juzi upande wa NCCR-Mageuzi.

Kwa hiyo, watu ni kama wamepoa hawajui cha kufanya. Yaani siasa zimewaparaganisha watu. Haiishii hapo sisi tunatambua nguvu yetu kama chama cha kujitathmini, kujiangalia tufanye nini.

Tulikuwa tuna mpango mkakati ambao uliishia 2020 na sasa hivi tumeshajitathmini na tumejiangalia upungufu wetu, ni maeneo gani ambayo tunahitaji kuimarika zaidi na ni yapi ambayo tunatakiwa kufanya kazi bora zaidi.

Sasa tupo kwenye mpango wa kutengeneza mkakati mwingine ambao ninaamini utaonyesha sura halisi ya ACT pande zote za Muungano na hili suala kama Bara tumejificha basi tutaonekana na tutatumia nyanja zote.

**SWALI:** Mwaka 2015 chama chenu kilisimamisha mgombea urais mwanamke. Tutegemee hilo katika uchaguzi mkuu ujao?

**JIBU:** Kwanza kitu muhimu cha kujua ni kwamba ACT ni chama ambacho hakijampa mwanamke fursa bali kimemwezesha na kumpa fursa ya kukua kisiasa na hii ni muhimu sana kwa wanawake hasa tunapochagua vyama.

Mama Anna Mghwira, Mungu amrehemu, alikuwa mwanasiasa wa siku nyingi na hakuwahi kuchanua kama ilivyotokea kwa ACT.

Tuliona alivyofanya kazi vizuri hadi kuwa mgombea urais kupitia ACT-Wazalendo. Kwa hiyo, tutegemee kuwaona wagombea urais wanawake, lakini hili ni suala linalopitia taratibu za chama.

**SWALI:** Ajenda kuu ya ACT-Wazalendo kwa wananchi ni ipi katika awamu hii ya Rais Samia?

**JIBU:** Ajenda kubwa tangu ACT inaanzishwe ni kuwa chama cha wananchi, kinachowapa majibu ya kuwa Watanzania, ndio maana kikapewa jina la Wazalendo na kuwapeleka kwenye maisha bora ambayo kila Mtanzania anayatamani.

Kwa hiyo, ajenda yetu bado ni kufikiwa, kusemewa changamoto za kila siku za mwananchi wa kawaida. Mfano, hivi sasa mwananchi wa kawaida anapogeuka anakutana na tozo, kila kitu kimezuiliwa.

Kwa hiyo, ni kuendelea kuwa karibu na mwananchi na kuwasemea na kuikumbusha serikali kila wakati kwa kuleta sera na taratibu ambazo zitamkomboa mwananchi ili aweze kuishi kwenye nchi yake akichanua na kufanya maendeleo kama mtu huru na mtu ambaye ana haki ya kutukuzwa kwa sababu kazi yetu ya msingi sasa hivi kama chama mbadala ni kuikosoa serikali.

> “Sasa tupo kwenye mpango wa kutengeneza mkakati mwingine ambao ninaamini utaonyesha sura halisi ya ACT pande zote za Muungano na hili suala kama Bara tumejificha basi tutaonekana na tutatumia nyanja zote.

Tunaipa serikali mawazo mbadala ndiyo maana unaona sisi ni chama ambacho tunasemea kila suala.

Ndiyo maana juzi tulisemea mambo ya tozo, ya miamala ya simu, kodi ya majengo na tumeipa serikali namna mbadala ili wafanye mambo yaende vizuri.

Lakini kwa upande mwingine, hatutabaki nyuma kutetea uwapo wa katiba bora ya wananchi inayotokana na Watanzania wenyewe.

**SWALI:** Serikali imetangaza kufanya marejeo katika tozo za miamala ya simu. Nini msimamo wa ACT-Wazalendo kuhusu hili?

**JIBU:** Msimamo ni ule ule, hii siyo kodi, ifutwe. Serikali itafute vyanzo vingine bora ambavyo havitampa shida mwananchi, tupo hapa kwa ajili ya watu wa kawaida.

Kwa hiyo, kutokana na hizi kodi nimesikia wanaofanya kazi kwenye kampuni za simu, biashara imepungua. Hata mimi nimepunguza kutuma pesa.

Kama sina sababu nitatumia njia ambayo itanipa ahueni, unakatwa kodi kwa kutuma pesa kidogo taribani Shilingi 5,000 au 6,000.

Kwa mtu wa kawaida hayo ni matunda ya wiki nzima. Kama ni hela ya mtoto shule mia tano hizo ni za wiki mbili.

Kwa hiyo, msimamo wetu ni pale pale, kodi iondolewe. Sisi tunasema serikali iondoshe mzigo, iendelee kupunguza mizigo kadri iwezekanavyo kwa mwananchi wa kawaida.

**SWALI:** Katika mazungumzo umegusia katiba mpya, lakini hivi karibuni tumeona CHADEMA wakifanya makongamano mikoani ambayo yalizuiwa na dola. Ninyi mna mikakati ipi katika kudai katiba mpya?

**JIBU:** Kwanza; kama unavofahamu sisi tumekubali katiba mpya na tunahitaji katiba mpya ya wananchi.

Katiba ni zao la matakwa ya wananchi na kwamba tunaendaje kutoka hatua hii kwenda nyingine. Na tunaamini kwamba wananchi ndiyo wanatakiwa washirikishwe, wafuatwe waulizwe wanataka nini kwenye katiba na kipi hawakitaki.

Pia tunaamini kwamba njia zote chanya za kuleta katiba mpya zipewe nafasi zizungumze. Kwa vile tu chama tawala kinaona kwamba huu si wakati wake labda, haina maana kwamba haturuhusiwi kuongea, tunaruhusiwa.

Kama nilivyosema, tumefanya tathmini ya mambo yetu ya ndani ya chama, ya nje, ya, ya kisera, msimamo na yale ambayo tunatakiwa kuendelea kuelimisha na kufanyia kazi.

Chama cha siasa jambo letu siyo tu kukosoa serikali, pia ni wajibu wetu kama Watanzania kuwaelimisha wananchi mambo ambayo ni ya msingi kama hilo la katiba mpya.

Kwa hiyo, tutakuwa sehemu ya kufanya hilo na tutakuja na mkakati.

**Imeandaliwa na Haika Christopher (SJMC) Layla Joho (TUDARCo) na Sechellah Nakamba (SJMC)**

## HIBATULLAH AKHUNDZADA

# Kiongozi mpya Afghanistan aliyejitokeza kwa kishindo kusimamia dini na serikali

**Na Ani Jozeni**

SIKU chache baada ya majeshi ya Marekani kuondoka Afghanistan, utawala mpya ambao umerudi madarakani baada ya miaka 20 ya mapigano na Marekani na serikali dhaifu iliyoiweka jijini Kabul, umeanza kuonekana bayana.

Hibatullah Akhundzada ndiye kiongozi mkuu wa kidini , akiwa na mamlaka ya juu ya Taliban wananchi humtambua kwa jina la Amir al-Mu'minin.

Akhundzada ni mwenye msimamo mkali, ni msomi wa dini kutoka Kandahar, jiji la pili kwa ukubwa nchini Afghanistan. Katika miaka ya 1980, Akhundzada alihusika kwenye upinzani dhidi ya uvamizi wa Soviet nchini Afghanistan. Lakini akaibuka kuwa kiongozi wa kidini zaidi kuliko mwanajeshi na mpigania uhuru.

Anatajwa kuwa jaji mkuu. Wataliban wanasimamia msimamo mkali wa sharia, kuwa mzinzi adhabu yake ni kifo wakati mwizi anakatwa mikono. Akhundzada anaripotiwa kuwa alitoroka Pakistan mwaka 2001, baada ya Marekani kuingilia kati kuliondoa kundi la Talban madarakani.

Yako maeneo mawili ambayo yamegusa wachambuzi nchi za nje, kuwa kimsingi kiuongozi nchi hiyo itafanana na utawala wa Iran, kuwa kiongozi wa dini anakuwa ndiye kiongozi mkuu anayeteuliwa na baraza la juu la maulamaa, halafu kuna kiongozi wa serikali anayetokana na idara ya siasa ya kundi hilo, ambaye ni Abdul Ghani Baradar, ndiye anayefahamika zaidi na aliingia kwa ulinzi mkali.

Kuna changamoto iliyojitokeza katika kipindi cha mpito, kati ya kuondoka kambini kwa majeshi ya Marekani na kupeleka kikosi maalum cha askari 5,000 uwanja wa ndege wa Kabul, kufanikisha kuondoka kwa maelfu ya raia wa Marekani na wasaidizi wao.

Zaidi ya watu 20,000 tayari walishaondolewa nchini humo na inaelekea ni zaidi ya hapo, kwani Marekani ilikuwa inatumia ndege kadhaa za mizigo kuondoa mamia kwa mamia ya watu kila safari, zikiwa tano hadi nane kwa siku. Jitihada ya vyombo vya habari vya Marekani na nchi nyingine kujua bado wageni wangapi wamebaki ziligonga mwamba, kwani wengine wanaingia kinyemela bila kuarifu serikali au balozi zao.

> “Kundi hilo limechukua nafasi ya Al Qaeda, ambayo ilidhoofishwa na kuuawa kwa wasaidizi wote wa karibu wa kijeshi wa Osama Bin Laden halafu yeye mwenyewe, na miaka ya karibuni Marekani ilitangaza kumuua mwanaye Osama katika shambulio la anga.

Taliban ilimtangaza Haibatullah Akhundzada, kiongozi mkuu wa kidhehebu mkuu wa nchi na wachambuzi wanasema ni mtu mwenye msimamo wa sharia usiotetereka, umri wake umeshapita miaka 60. Alichukua usukani wa uongozi baada ya mtangulizi wake, Mullah Akhtar Mohamed Mansour, kuuawa katika shambulio la droni (ndege isiyo na rubani) mwaka 2016. Ndiye ambaye atakuwa na neno la mwisho kwa masuala yote ya kisiasa, kijeshi na kidini nchini Afghanistan, kama ilivyozoeleka.

Kundi hilo linasema litaunda serikali yenye ushirikishwaji mpana, ikiwalenga walioshiriki angalau kwa mbali katika utawala uliopita, akiwamo rais wa zamani wa nchi hiyo, Hamid Karzai, ambaye alichukua madaraka kwa msaada wa Marekani ilipoingilia kati 2001 baada ya shambulizi la New York likiongozwa na Osama bin Laden.

Rafiki huyo wa Taliban alikuwa amejichimbia nchini Marekani ikataka akabidhiwe kwao, ili ajibu mashtaka ya mauaji na ugaidi, serikali ya Taliban ikataka ipewe ushahidi ndiyo imtoe.

Karzai amekuwa na mazungumzo na viongozi wapya kuhusu ushiriki wa makundi tofauti, ili amani iweze kurudi chini ya uongozi mpya, badala ya kujenga mifarakano ndani ya taifa lao halafu na nchi za jirani, kuzuia hali ya amani katika nchi yao isitengemae, wakimbizi kuongezeka na si ajabu vita kuanza tena. Walipokamilisha kuteka jiji la Kabul, wasemaji wa Taliban wanasisitiza katika mkutano na waandishi wa habari wa mashirika mbalimbali, wakati huo Marekani ikiendelea kuondoa watu wake na raia waliowasaidia, kuwa hawatalipa kisasi.



Kiongozi mkuu wa kiserikali na kidini wa Afghanistan Hibatullah Akhundzada. **PICHA: MTANDAO.**

Baadhi ya mashirika ya habari likiwamo jarida la Foreign Policy (siasa za nje) la Marekani yalisema walioshirikiana na serikali iliyopita wanatafutwa na akikoswa, ndugu yake atauawa.

Kielelezo cha ugumu wa kuunda serikali shirikishi siyo tu hasira ya kundi hilo kwa washirika wote wa Marekani, ila undani wa tofauti zilizoko miongomi mwa washirika katika kupambana na Marekani, kwa mfano kundi la Islamic State.

Kundi hilo limechukua nafasi ya Al Qaeda, ambayo ilidhoofishwa na kuuawa kwa wasaidizi wote wa karibu wa kijeshi wa Osama Bin Laden halafu yeye mwenyewe, na miaka ya karibuni Marekani ilitangaza kumuua mwanaye Osama katika shambulio la anga.

Kundi la Islamic State lina msimamo mkali kuliko Taliban, na lilifanya shambulio uwanja wa ndege wa Kabul wakati operesheni ya kuondoa watu inaendelea. Marekani ikitumia mtandao wake wa ujasusi iliigundua nyumba ya kiongozi wao, hapo Kabul ikaishambulia kwa bomu lililotupwa na ndege ya droni na kutangaza kuwa aliuawa. Hapakuwa na shambulio baada ya hapo.

Bado Taliban ina changamoto kubwa ya kuweka nchi katika hali ya usalama na kujaribu kusimamia uchumi, ili taifa hilo lisimame wima, chakula, dawa na huduma nyingine za kijamii vipatikane na uzalishaji uendelee licha ya kuwa wasomi wengi wameondoka na baadhi wanajaribu kutoroka kokote pale, ambapo wanaona mpaka unapitika.

Nchi za nje zimepata mtihani mkubwa kukubali wakimbizi kutoka Afghanistan licha ya juhudi za Marekani kuwatafutia, kwani makundi ya siasa Ulaya yanaamini wataingia na 'virusi' vya siasa kali licha ya kukimbia vita, kama ilivyotokea kwa wakimbizi wa Syria na Iraq miaka iliyopita.

Kuna mkwamo mkubwa wa kimaisha na huduma za jamii kwa kuzuiwa kutumia rasilimali za nje hadi utokee utawala unaotambuliwa na nchi za Ulaya na Marekani. Ni China, Russia na Iran ndiyo zinaonyesha kushabihiana na utawala mpya wa Taliban.





## Sera ya wazee sasa mbioni

**Na Paul Mabeja,** MANYONI

SERIKALI ipo katika hatua za mwisho za mapitio ya Sera ya Wazee ya mwaka 2003, ikiwa ni hatua ya kutimiza azma ya kuimarisha afua mbalimbali kwa wazee nchini.

Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, aliyasema hayo juzi katika kijiji cha Sukamahela wilayani hapa wakati akitoa taarifa kwa umma kuhusu maadhimisho ya siku ya kimataifa ya Wazee Duniani Oktoba 1.

Dk. Gwajima alisema masuala yatakayozingatiwa katika sera hiyo ni huduma za afya, matunzo, ulinzi na usalama, hifadhi ya jamii, maandalizi ya wananchi kuelekea maisha ya uzee na msaada wa kisaikolojia yamewekewa mikakati madhubuti ili kuhakikisha wazee wanapata huduma jumuishi na stahiki kwa ajili ya ustawi na maendeleo yao.

"Vilevile serikali kwa kushirikiana na wadau imeendelea kutekeleza afua mbalimbali zinazalenga katika kutatua changamoto mbalimbali zinazaowakabili wazee," alisema Dk. Gwajima.

Kuhusu maadhimisho hayo, Waziri huyo alisema kwa mwaka huu yataambatana na huduma mbalimbali ikiwamo kupimwa maradhi mbalimbali kama vile shinikizo la damu, kisukari na tezi dume.

Dk. Gwajima alisema pia zitatolewa huduma za msaada wa kisaikolojia na elimu kuhusu kujikinga na ugonjwa wa UVIKO-19 pamoja na kuhamasisha wazee na wananchi kupata chanjo.

"Halikadhalika kuelekea siku ya kilele cha maadhimisho hayo mwaka huu nchini wazee watapata fursa ya kukutana na kujadili mambo mbalimbali yanayohusu maisha yao na kuweka mapendekezo ya namna bora ya kushughulikia changamoto zinazowakabili," alisema.

Alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuongeza uelewa wa jamii kuhusu masuala mbalimbali ya wazee ikiwa ni pamoja na kutafakari fursa na kero zinazowakabili na namna ya kuzitatua.

"Hivyo ni wajibu wetu kama taifa kutumia siku hii kutambua machango wa wazee na kuwaenzi ipasavyo kwa kulinda, kuhifadhi, kukuza na kuimarisha upatikanaji wa haki zao katika jamii," alisisitiza Dk. Gwajima.

Alieleza kuwa maadhimisho hayo yatafanyika katika ngazi za mikoa na maelekezo tayari yametolewa kupitia Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) huku Wizara itashiriki wilayani Mpwapwa.

"Kauli mbiu ya maadhimisho kwa mwaka huu inasema 'Matumizi sahihi ya kidigitali kwa ustawi wa rika zote', ujumbe huu umewekwa mahususi ili kusisitiza umuhimu wa kutoa nafasi kwa wazee kushiriki katika matumizi ya kidigitali ili kutatua changamoto mbalimbali na kufanya shughuli za ubunifu katika kujiletea maendeleo," alisema.

Alisema taarifa ya Umoja wa Mataifa katika masuala ya mawasiliano ya mwaka 2019, inaonyesha kuwa wanawake na wazee ndio makundi ambayo yameachwa nyuma katika matumizi ya digitali.

# Waziri Ndalichako aonya udanganyifu wa mtihani darasa 7

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, amewaonya wasimamizi wa mtihani wa taifa wa darasa la saba unaotarajiwa kuanza leo kujiepusha na udanganyifu. Prof. Ndalichako aliyasema hayo jijini hapa kwenye ziara yake ya kutembelea ujenzi wa Shule ya Sekondari ya mfano ya Iyumbu.

Alisema katika miaka miwili iliyopita kumekuwa na tabia ya udanganyifu wa mitihani unaofanywa na wasimamizi kwenye shule mbalimbali na kuwataka kufanya kazi hiyo kwa kuzingatia maadili na miiko ili kutochukuliwa hatua za kisheria.

"Naomba wasimamizi wote mfanye kazi ya usimamizi kwa weledi ili wanafunzi watahiniwa wafanye mitihani sahihi kwa kutumia akili zao na uwezo waliofundishwa darasani," alisema.

Aliwataka wanafunzi wanaofanya mtihani huo kujiamini wanapoingia katika mitihani hiyo ili kufanya vizuri na kupata ufaulu mkubwa.

Kuhusu, ujenzi wa shule hiyo, Waziri Ndalichako aliagiza ujenzi huo kukamilika kabla ya mwezi Februari 2022 ili ipokee wanafunzi wa kidato cha kwanza.

"Hii shule ni nzuri sana kwa sababu ina kila kitu ikiwamo maabara na sehemu za michezo na vitu vingine ambavyo vinahitajika kuwa katika shule," alisema Prof. Ndalichako.

Alisema shule imetumia Sh. bilioni 17 kwa ajili ya ujenzi ni bora ambayo mwakani inahitajika kuanza kutumika na wanafunzi hao. Pia, alisema serikali imepanga kujenga shule 10 za mfano katika mikoa 10.

Alisema hivi sasa wako katika hatua za mwisho za kukamilisha kuhamisha fedha kwenda katika halmashauri zao kwa ajili ya ujenzi wa shule hizo.

Naye, Msimamizi wa ujenzi shule hiyo, Luteni Kanali Philemon Komanya, alisema ujenzi wa shule hiyo umefikia asilimia 60 na kuahidi kukamilisha kwa muda uliopangwa kwa mujibu wa mkataba.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako (katikati), akikagua ujenzi wa madarasa na nyumba za walimu katika shule ya sekondari ya mfano ya Iyumbu, jijini Dodoma juzi. Kulia kwake ni Msimamizi wa mradi huo, Luteni Kanali Philemon Komanya. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Waziri akemea matamko kwenye nyumba za ibada

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

SERIKALI imewataka viongozi wa dini kujiepusha na migogoro na kutoa matamko, ambayo yatasababisha uvunjifu wa amani.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki, jijini hapa kwenye ibada ya kumweka Wakfu Askofu Mkuu Msaidizi wa Kanisa la Pentekoste Renew Assembly (PRA).

Alisema viongozi hao wanapaswa kutumia nyumba zao za ibada kuzungumza habari za upendo na amani, kuepuka kutoa matamko yanayoleta mgawanyiko kwenye jamii na waumini wao.

"Sisi wananchi tunawaamini sana ninyi viongozi wa dini, lakini ikitokea migogoro kati yenu inatuchanganya, kwa sababu tunaamini mnayajua vizuri maandiko matakatifu ya Mungu na jinsi ya kuvumiliana na kuishi kwa upendo," alisema.

Waziri Simbachawene alizitaja baadhi ya sababu za migogoro mingi iliyopo katika taasisi za kidini kuwa ni inayosababishwa na kugombea madaraka au fedha.

Alibainisha kuwa sababu hizo na zingine zimekuwa zikisababisha kuwagawa waumini wao na kusababisha uvunjifu wa amani .

Aidha aliwakemea baadhi ya viongozi wa dini ambao wamekuwa wakitumia vibaya nyumba hizo za ibada kutoa matamko, ambayo yanaleta mgawanyiko katika jamii.

Alisisitiza kuheshimu sheria, kwa sababu kila dhehebu la dini limesajiliwa kwa madhumuni ya kutoa huduma zilizokusudiwa na sio kusababisha migogoro.

Kwa upande wake, Askofu Mkuu wa Kanisa hilo, Wilson Mwaoga, alisema ibada hiyo ilikuwa maalum, kwa ajili ya kumweka Wakfu Askofu Mkuu Msaidizi wa Kanisa hilo, Emmanuel Mogope.

Askofu Mwaoga alisema katika ibada hiyo waliwaalika watu wachache, kutokana na kuchukua tahadhari ya maambukizi ya ugonjwa wa UVIKO- 19.

Alisema kanisa hilo lina matawi mengi nchini na nje ya nchi ambao walitamani kufika, uwapo wa ugonjwa huo uliwazuia kufika.

Aidha aliomba serikali kusaidia migogoro inapojitokeza, ili kuepuka kusababisha uvunjifu wa amani

Kadhalika aliomba mabaraza ya kidini kusaidia kusuluhisha migogoro inapojitokeza kwenye maeneo yao.





# Watoto matatani kwa tuhuma za kukutwa na noti za bandia

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

JESHI la Polisi mkoani Mbeya, linawashikilia watoto wawili kwa tuhuma za kukutwa na noti bandia 13 za Sh. 10,000 ambazo zingekuwa fedha halali zingekuwa na thamani ya Sh. 130,000.

Fedha hizo zinadaiwa zilikuwa katika mpango wa kuingizwa kwenye mzunguko kwa kununua bidhaa mbalimbali.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Mbeya, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Ulrich Matei, alisema hayo jana alipokuwa anazungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio mbalimbali ya kihalifu mkoani hapa.

Aliwataja watuhumiwa hao kuwa ni Alen Ngai (17) na Jackson Godlove (17) wote wakazi wa Isanga jijini Mbeya na kwamba watoto hao walikamatwa juzi katika eneo la Sinde jijini hapa wakijiandaa kuzitumia fedha hizo.

"Watuhumiwa wanasubiri kufikishwa kwenye vyombo husika kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria. Vilevile tunaendelea na upelelezi ili tujue wanaoshirikiana na watoto hao kwenye mtandao wa fedha hizo," alisema Kamanda Matei.

Katika hatua nyingine, Kamanda Matei alisema jeshi hilo linawashikilia walimu wawili kwa tuhuma za kutaka kuharibu mitihani ya darasa la saba inayotarajiwa kuanza kufanyika leo nchi nzima kwa kuiba mitihani na kuisambaza.

Kamanda Matei alisema majina ya watuhumiwa hao yanahifadhiwa kwa sababu ya kiupelelezi na kwamba kinara wa tukio hilo alikamatwa katika Kata ya Chimala wilayani Mbarali akiwa kwenye harakati za kutoroka kwenda Sengerema mkoani Mwanza.

Alisema mtuhumiwa baada ya kuhojiwa, alikiri kushiriki kwenye wizi wa mitihani tangu mwaka 2006 na kwamba amefanya kazi hiyo katika mikoa mbalimbali nchini.

Kwa mujibu wa Matei, walibaini kuwa mtuhumiwa huyo alipokea fedha nyingi kutoka kwa watu mbalimbali kwa ajili ya kufanikisha uhalifu huo wa wizi wa mitihani na kwamba amekuwa akizisaidia shule za watu binafsi zikiwamo za mchepuo wa Kiingereza.

"Tunazishikilia akaunti zake na fedha alizoingiziwa zinaonekana na sasa tunaendelea kufuatilia ili kuwabaini waliomwingizia fedha hizo. Nawataka walimu na wadau wote wanaohusika kwenye mitihani hii wasifanye udanganyifu wa aina yoyote," alisema Matei.

Alisema jeshi hilo litaendelea kufuatilia na endapo kiongozi yeyote ama mwalimu ama mzazi atakamatwa kwa kosa hilo la udanganyifu wa mitihani atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Matei aliwataka wanafunzi pia kufanya mitihani hiyo kwa uaminifu bila kushiriki kwenye vitendo vya udanganyifu kwa maelezo kuwa hata wao wakikamatwa watachukuliwa hatua kali za kisheria.




Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mbeya, Ulrich Matei, akionyesha kwa waandishi wa habari lita 2000 za mafuta ya petroli, zilizokamatwa zikisafirishwa kwenye gari aina ya Canter kinyume cha sheria, katika eneo la Ituta, jijini Mbeya jana. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# UWT yaanza ziara kutatua kero za kinamama

**Na Grace Mwakalinga** MBEYA

KAMATI ya Utekelezaji ya Jumuiya ya Umoja wa Wanawake Tanzania (UWT) Mkoa wa Mbeya imeanza ziara ya kutembelea na kubaini vikwazo vinavyowakabili wanawake na kero walizonazo hasa katika utekelezaji wa miradi ya jumuiya hiyo ili zitafutiwe ufumbuzi. Ziara hiyo ilianzia katika Wilaya ya Mbarali kwa kutembelea miradi saba iliyoko katika Kata ya Chimala.

Mwenyekiti wa UWT Mkoa wa Mbeya, Oliva Kibona, alisema lengo hasa ni kuangalia kama miradi inayoanzishwa inatekelezwa kulingana na fedha halisi.

"Tumeanza ziara kutembelea miradi yetu ya jumuiya, lakini tunapita kuwashukuru wanawake kwa kuendelea kukiamini Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kukipa ridhaa ya kuendelea kushika dola," alisema mwenyekiti huyo.

Kibiona alitaja baadhi ya miradi ambayo imetembelewa katika Wilaya ya Mbarali kuwa ni pamoja na kuangalia ujenzi wa nyumba ya katibu wa UWT wa wilaya, vyumba vya biashara na ukumbi ambao utatumika kama kitega uchumi cha jumuiya hiyo.

Naye Katibu wa UWT Mkoa wa Mbeya, Mary Mwasengo, alisema ziara hiyo pia inalenga kuhamasisha wanawake kujiunga na CCM na kujisajili kwenye mfumo mpya wa kielektroniki ambao unakiwezesha chama kujua idadi halisi ya wanachama.

"Tunapita kuhamasisha wanawake wajiunge na chama chetu na kuwashauri wahakikishe wanakuwa na kadi za uanachama za kielektroniki. Tunajua viongozi wenzetu katika wilaya wanaifanya sana hii kazi lakini tumekuja kushirikiana kuongeza nguvu na kama mnavyojua mwanamke ni jeshi kubwa," alisema.

Mjumbe wa Baraza Kuu ya UWT, Mary Mbwilo, alisema ziara hiyo pia inatoa elimu kwa wanawake namna ya kufaidika na mikopo inayotolewa na taasisi za umma ukiwamo mkopo unaotolewa na Wakala wa Huduma za Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili kutambua na kuzitumia fursa hizo.

# RC apigia debe ununuzi mahindi

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

MKUU wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, ameagiza Wakala wa Taifa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kupunguza ununuzi wa tani 400 za mahindi katika eneo la Vwawa Wilaya ya Mbozi na kuelekeza mahindi hayo yanunuliwe katika wilaya ya Mbozi.

Hatua hiyo inatokana na serikali kubaini kuwa wakulima wa Wilaya ya Ileje mkoani hapa wamezalisha mahindi kwa wingi katika msimu huu wa kilimo.

Agizo hilo alilitoa baada ya kufanya ziara ya ghafla katika soko la mahindi la Isongole, wakati akitokea kwenye ziara yake ya kazi ya kukagua miradi mbalimbali ambayo itatembelewa na Mwenge wa Uhuru mkoani hapa.

Mkuu huyo wa mkoa baada ya kufika katika soko hilo alibaini uwapo wa shehena kubwa ya mahindi, hivyo kuagiza NFRA kuongeza tani za ununuzi kwenye wilaya hiyo.

"Wilaya hii ilipangiwa tani 800 za mahindi ndizo zinunuliwe lakini kwa kuwa mahitaji ni mengi natoa maagizo haya. Wakati serikali inaangalia namna ya kuhakikisha wakulima wanapata soko la mahindi, nawaagiza NFRA kupunguza tani 400 ambazo mlipaswa kununua kwenye eneo la Vwawa mje mnunue huku kwa wakulima wa Isongole," alisema.

Wakulima hao wakiwamo Ubatizo Japioni na Mases Kayinga, waliishukuru serikali kwa kuamua kununua mahindi kwao lakini wakalalamikia hali ya soko kuwa bado ni changamoto kubwa na kuomba serikali kuongeza kiwango cha ununuzi.

"Mimi mwenyewe mahindi ninayo mengi sana hata hapa sijaleta kabisa. Masoko hakuna kabisa tunaomba serikali itusaidie kupata masoko," alisema Japioni.

Katika msimu huu wa kilimo, Mkoa wa Songwe ulizalisha mazao ya chakula tani milioni 1.4 wakati uhitaji ni tani 350,000 tu, hivyo mkoa kubaki na ziada ya chakula ya zaidi ya tani milioni moja.

Ili kuhakikisha wakulima hawapati hasara, Mgumba ametoa wito kwa wafanyabiashara nchini kuja mkoani hapa kununua mazao na kuyauza nje ya nchi kwa kuwa tayari serikali ilishafungua milango.

**"Mimi mwenyewe mahindi ninayo mengi sana hata hapa sijaleta kabisa. Masoko hakuna kabisa tunaomba serikali itusaidie kupata masoko," alisema Japioni.**





# Mufti achanja corona, atia neno

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MUFTI Mkuu wa Zanzibar Sheikh Saleh Kabi, ameongoza viongozi wa dini wa madhehebu mbalimbali kupata chanjo ya Covid -9, huku akisisitiza chanjo ni wajibu kwa ajili ya kupambana na maradhi hatari.

Mufti mkuu huyo jana aliongozana na viongozi wengine wa dini zaidi ya 30 kuchanja chanjo ya corona aina ya Johnson katika Hospitali ya Mnazi Mmoja Mjini Unguja.

Akizungumza na waandishi wa habari baada ya kupata chanjo hiyo, alisema chanjo ambayo inatolewa kwa madhumuni ya kinga ya maradhi mbalimbali inakubalika katika dini ya Kiislamu.

Alisema madhumuni ya chanjo ni kujikinga na maradhi hatari, ambayo yanaweza kusababisha vifo kwa jamii na kuambukiza watu wengine.

"Suala la chanjo halina matatizo, limeruhusiwa katika dini ya Kiislamu ikiwa ni kinga ya maradhi hatari yanayoweza kusababisha vifo kwa kundi kubwa la watu," alisema.

Naye Katibu Mtendaji wa Wakfu na Mali ya Amanam, Dk.Abdalla Talib Abdallah, alisema kutolewa kwa chanjo aina ya Johnson itawawezesha waumini wa dini ya Kiislamu wenye nia ya kufanya safari za ibada ya Hijja kutekeleza safari hiyo.

Alisema tayari ofisi ya Wakfu imepokea maombi mbalimbali ya taasisi nyingine za kidini kutaka kusafirisha waumini wao katika ibada ya Umra huko Sauda Arabia.

Alieleza kuwa kwa mujibu wa masharti ya ibada ya Umra pamoja na hijja, hakuna Muislamu atakayeruhusiwa kutekeleza ibada hiyo bila kupata chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona.

"Chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona haizuiliki kwa waumini wa dini ya Kiislamu wenye nia ya kufanya ibada ya Umra pamoja na hijja nchini Sauda Arabia," alisema.

Padri Magamba Michael wa Kanisa katoliki Machui Wilaya ya Kati Unguja ni miongoni mwa viongozi wa dini waliojitokeza na kupata chanjo hiyo na kusema chanjo ni muhimu katika kupambana na kujikinga na maradhi hatari yanayoweza kusababidsha vifo.

"Nawaomba waumini wa dini ya Kikristo kujitokeza kupata chanjo ambayo itasaidia kujikinga na maradhi hatari yanayoweza kusababisha vifo na kupoteza taifa nguvu kazi," alisema.



Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Dk. Omar Dadi Shajak, akizungumza na ujumbe kutoka Ofisi ya Waziri Mkuu, Migombani Mjini Zanzibar juzi. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Masheha wapewa jukumu la elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MASHEHA Mkoa wa Kaskazini Unguja, wametakiwa kuhakikisha katika shehia zao hakuna mtoto ambaye hajapelekwa shule wakati ameshafikisha umri wa kuhudhuria shule.

Hayo yalisemwa jana na Mkuu wa Mkoa huo Ayoub Mohamed Mahmoud wakati akizungumza na Masheha kuhusu utekelezaji wa mradi wa kuwarudisha shule watoto waliotoroka na wengine kujiingiza katika ajira za kutembeza watalii na uvuvi.

Alisema malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni kuhakikisha watoto waliofikisha umri wa kwenda shule wanapata elimu kwa mujibu wa sheria na hakuna mtoto aliopo nje ya mfumo wa elimu ya lazima.

Aidha alieleza kuwa kipaumbele cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni sekta ya elimu na ndiyo maana mara baada ya Mapinduzi ya Januari 12 mwaka 1964 serikali ilitangaza elimu bila ya malipo kwa watoto wote wa wakulima na wafanyakazi.

"Masheha wote wa mkoa wa Kaskazini Unguja mhakikishe watoto waliofikisha umri wa kwenda shule wanapata haki ya elimu na waliotoroka wanarudishwa mara moja," alisema.

Naye Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Ali Khamis, alisema wizara imekusudia kuwarudisha shule watoto 35,732 ambao wapo nje ya mfumo wa elimu ya lazima.

Khamis alisema kuwapo kwa nje ya mfumo wa elimu kwa watoto hao ambao wametoroka kwa kiasi kikubwa wamekosa moja ya haki ya msingi ya elimu ya lazima inayotolewa na Wizara ya elimu.

Aliyataja matarajio ya kufanikishwa kwa zoezi yapo kwa masheha wa shehia mbalimbali na kwamba kwa kiasi kikubwa wao ndiyo wenye jukumu na uwezo wa kuwatambua watoto waliotoroka shule.

"Mafanikio ya mradi huu kwa asilimia kubwa yatategemea ushirikiano utakaoonyeshwa na masheha wa shehia mbali mbali za Mkoa wa Kaskaini Unguja ambapo watoto hao wapo," alisema.

Mkurugenzi Mendaji wa Taasisi ya Elimu kwa Wote (EAC) wanaotekeleza mradi huo, Mary Pigozzi, alisema wamejipanga kusimamia mradi huo kuona watoto wenye haki ya kupata elimu wanarudishwa shule.

Aidha, alifurahishwa na juhudi zilizochukuliwa hadi sasa ambapo watoto 4,809 wamerudishwa shule na kuendelea na masomo.

"Taasisi yetu imejipanga kuhakikisha watoto wanarudishwa shule na kuendelea na kupata elimu ambayo ni haki ya msingi ya maendeleo la taifa"alisema.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inatekeleza mradi wa kuwarudisha shule watoto waliotoroka wanaofikiwa 35,732 kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu, Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto (UNICEF) na Taasisi ya kimataifa ya Elimu kwa wote ya Qatar (EAC).

# Jaji Mkuu: Wanasheria tokomezeni udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JAJI Mkuu wa Zanzibar, Omar Othman Makungu, amewataka wanasheria kutumia taaluma zao kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Jaji Makungu alisema hayo katika mahafali ya tano ya wanafunzi wa kituo cha sheria Mjini Unguja.

Alisema vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia ni moja ya tatizo kubwa ambalo limeufanya uongozi wa Mahakama kukutana na kulijadili mara kwa mara na kuitisha vikao kwa ajili ya kulipatia ufumbuzi.

Makungu alisema kuanzishwa kwa Mahakama Maalum ya kusikiliza kesi za udhalilishaji wa kijinsia ikiwemo ubakaji ni hatua nzuri ambapo sasa mahakimu wamekuwa wakitoa hukumu katika kipindi kifupi, hatua ambayo imesaidia kupunguza malalamiko ya wananchi.

"Tumeanza kusikiliza kesi za udhalilishaji kwa kasi kubwa na kuzitoleya hukumu haraka, hatua ambayo imesaidia kwa kiasi kikubwa kupunguza malalamiko yaliyokuwepo katika jamii ya kulalamika kesi kuchelewa kusikilizwa na nyengine kufutwa bila kujulisha wahusika," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Taasisi ya Kituo cha Sheria, Muumini Khamis Kombo, alisema chuo hicho kilianzishwa mwaka 2014 na kimeshatoa wahitimu 75 katika ngazi mbalimbali ya cheti na diploma na wengine kufanyakazi katika taasisi mbalimbali za serikali na sekta binafsi.

Alisema taaluma ya sheria bado mahitaji yake ni makubwa nchini, ambapo wahitimu wametakiwa kuitumia kwa ajili ya kufikisha elimu kwa wananchi na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili.

"Nendeni mkatumiye taaluma yenu kufikisha elimu ya sheria na kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazowakabili wananchi, hivyo kuwasaidia na kuwatatulia matatizo yao," alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais (Katiba , Sheria na Utawala Bora), Shaaban Seif Mwinyi, alisema serikali imefungua fursa kwa taasisi na watu binafsi kufungua taasisi zitakazotoa elimu ya sheria, ambayo mahitaji yake ni makubwa.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HALIFA SHABANI HOZZA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya bajaji boxer yenye namba za usajili **MC 551 CVN**,chasis namba **MD 2B 15BX8MWK90921**, yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

Polisi taarifa **DAR/CEN/RB/419860/2021**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**Fred Elias Mtei**

Mtajwa ni mkazi Ilembo Manispaa ya Mpanda Mkoani Katavi anatangaza kupotelewa na Kadi ya Pikipiki ya Tairi Tatu yenye Umiliki wa Tanzania China Trade yenye Namba za Usajiri **MC 594 CPN.** Yenye Rangi ya Kijani nimeripoti katika kituo cha Polisi cha Wilaya ya Mpanda nakupewa. **KAT/MPA/RB/435221/2021**

Kwa mtu yeyote ambae ata iona au kuiokota aipeleke katika kituo cha Polisi kilicho karibu nae au kwenye ofisi ya Mtaa/ Kijiji/ Kata

116446002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CHRISTIAN CHRISTOPHER** MWAKABANGO ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T.634 ACM** CHASSIS NAMBA **JALFTR32FR3000035** ENGINE NAMBA **823916.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.

TAARIFA YA POLISI **MBE/MBE/RB/435955/2021**

116446102

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi NO.263/2021**

**Ombi la MAGRETA JOHN KIOGWA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu ZACHARIA ALOYCE MOLLE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo tarehe 01/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 01/09/2021

Tarehe 1/9/2021
Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI MOROGORO

116446202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 52/2019**

**(Asilia Shauri la Jinai Na. 294/2017, Mahakama ya Wilaya ya Mtwara)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA.......................MRUFANI**

**DHIDI YA**

**HAMISI MOHAMED KAZUMARI...............MJIBU RUFAA**

**KUITWA SHAURINI**

**KWA: HAMISI MOHAMED KAZUMARI – NAMYAMBA MTWARA**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama kuu Mtwara kusikiliza rufaa hii mnamo tarehe 13/09/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi rufaa hii itasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 28/7/2021.

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

116446302

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA KUU MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA. 88/2019**

**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA**

**SHAURI LA MAOMBI NO. 11/2019**

**THE DPP..........................................APPELLANT**

**VERSUS**

**KASIMU ALLY.................................RESPONDENT**

**KWA: KASIMU ALLY - MTWARA**

**KUITWA SHAURINI**

Hii ni kukutaarifu kuwa unaamriwa kufika mbele ya Mahakama kuu Mtwara kusikiliza shauri hili mnamo tarehe 13/9/2021 saa 2:30 asubuhi bila kukosa.

Kumbuka kuwa endapo hutafika wewe mwenyewe au mtu yeyote anayeruhusiwa kisheria kukuwakilisha, basi shauri hili litasikilizwa na kuamriwa bila ya wewe kuwepo.

Imetolewa kwa amri yangu na kwa muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 30/7/2021.

A.H. MSUMI
NAIBU MSAJILI MFAWIDHI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MTWARA

116446402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA YA JINAI NA 62/2019**

**ASILIA MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA JINAI NO.29/2017**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA .........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**AGNES SEVERINE.........MRUFANIWA**

**DADI SALUM NAMKUDU.......MRUFANIWA**

**KWA.AGNES SEVERINE**
**MBAE MASHARIKI**
**MTWARA**
**DADI SALUMU NAMKUDU**
**MAGOMENI 'B'**
**MTWARA**
**KUITWA SHAURINI**

HII NI KUWATAARIFU KUWA MNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUTAJWA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 20/09/2021 SAA2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA,BASI SHAURI HILI LITASIKILIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 28/09/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI MFAWIDHI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
KANDA YA MTWARA

116446502

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MTWARA**

**SHAURI LA RUFAA NA.115/2020**

**(ASILIA JINAI 39/2020MAHAKAMA YA WILAYA MTWARA)**

**MKURUGENZI WA MASHITAKA.........MRUFANI**

**DHIDI YA**

**MOHAMED SALUM KOWEKA.........MJIBU RUFAA**
**KUITWA SHAURINI**

**KWA,MOHAMED SALUM KOWEKA**
**C/O SHARIFA MOHAMED KOWEKA**
**SIMU 078774775/0787327958**
**BOX MIEMBENI**
**MTWARA**

HII NI KUKUTAARIFU KUWA UNAAMRIWA KUFIKA MBELE YA MAHAKAMA KUU MTWARA KUSIKILIZA SHAURI HILI MNAMO TAREHE 27/09/2021 SAA 2:30 ASUBUHI BILA KUKOSA

KUMBUKA KUWA ENDAPO HUTAFIKA WEWE MWENYEWE AU MTU YEYOTE ANAYERUHUSIWA KISHERIA KUKUWAKILISHA ,BASI SHAURI HILI LITASIKLIZWA NA KUAMRIWA BILA YA WEWE KUWEPO

IMETOLEWA KWA AMRI YANGU NA KWA MUHURI WA MAHAKAMA LEO HII TAREHE 02/09/2021

A. H. MSUMI
NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MTWARA

116446602

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA BUKOBA MJINI**

**USIMAMIZI YA MIRATHI NA. 52 / 2021**

**Msimamizi wa mirathi Justina Kokwenda Elias**

**Msimamizi wa mirathi ya Prof. James Elias Lwelamira.**

Kwa kuwa Justina Kokwenda Elias amefungua kesi ya mirathi katika mahakama hii, watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 04/10/2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

SAHIHI YA HAKIMU

116446802

**Magistrates Court( Approved Forms For the Primary Court)**

**GN. NO 943 (Contd.)**

**FOMU MADAI -3**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo Wilaya ya Moshi**
**Kituo cha URU Mkoa Kilimanjaro**
**Shauri la Madai /Ndoa Na 01, 2021**
**Jina la Mdai Dativa Temba**
**Jina la Mdaiwa Godfrey P. Mushi**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

(Kanuni ya 18 kanuni za taratibu Madai katika Mahakama za Mwanzo)

Kwa: Godfrey P. Mushi

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta /Wameleta madai yake /yao kwamba (Eleza hapa habari za Madai )

**MADAI YA TALAKA**

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika mahakama hii tarehe 20 mwezi 9 mwaka 2021 saa 03:00 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri ni lazima kuleta shahidi/mashaidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shauruni,Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya w ewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 06 mwezi 09 mawaka 2021

...............................

**HAKIMU**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE**
**NO.84 OF 2021**
**In the Matter of the Estate of the late ELIAS MAJOGORO KUBOJA of MBWANGA Area within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY EVELYNE ELIAS MAJOGORO**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules Gn.369 Of 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 6TH day of OCTOBER 2021.

Dated at Dodoma this **20TH day of AUGUST 2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA MOROGORO**
**MOROGORO**

**SHAURI LA MADAI NA. 36 YA 2016**

**WINNIE BARAKA KIANGI............MSHINDA TUZO**

**DHIDI YA**

**SR. BLANDINA THOMAS SEMBU.........MSHINDWA TUZO**

**WITO WA MAHAKAMA**

**KWA: SR. BLANDINA THOMAS SEMBU**

WITO huu ni wa kesi tajwa hapo juu, ambayo imepangwa kutajwa kwa utekelezaji tarehe 4 mwezi wa 10 mwaka 2021 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mahakama ya Hakimu Mkazi Morogoro.

Unatakiwa kuhudhuria wewe binafsi au wakili au mtu yeyote alieidhinishwa kusimama kwa niaba yako na pia unatakiwa kutoa maelezo yako siku hiyo nakala zote za ushahidi utakazotumia kwa nini utekelezaji usiendelee dhidi Yako.

Zingatia kwamba, kutohudhuria siku ya kesi na kwa wakati uliotajwa hapo juu, Mahakama itaendelea na kusikiliza shauri hili na kutoa maamuzi bila ya uwepo wako.

Imetolewa chini ya muhuri wa Mahakama leo siku ya tarehe 2 mwezi wa 9 mwaka 2021

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI MWANDAMIZI
MOROGORO

116447302

## KUPOTEA KWA CHETI

**CHAMA CHA HUDUMA MAENDELEO KITENDAGURO** kinatangaza kupotelewa na cheti **CERTIFICATE OF REGISTRATION** yenye namba za usajili **NO:SO.11304** kilichotolewa na **WIZARA YA MAMBO YA NDANI mwaka 21st APRIL ,2002,**yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi

**Polisi taarifa JNIA/IR/LR/RB/NO.294/2019**

## TANGAZO KUPOTEA OFA YA KIWANJA

Juma Jumanne Anatangaza kupotelewa na Ofa ya kiwanja Namba 109/4 Kitalu "HH" (HD) kilichopo maeneo ya Ndala Manispaa ya Shinyanga. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu au awasiliane na Juma Jumanne kwa simu namba 0742450920.Rb namba/ SHY/RB/2021/Control namba 9910823669390.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**MODEV ENTERPRISES.CO.LIMITED** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **SANLG .(NYEKUNDU.)** yenye namba za usajili **MC 390 CRM. CHASIS NAMBA LBRSPJB51L9004931,ENGINE NAMBA 20909918,**yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi polisi taarifa RB,No. **GEI/CHA/RB/346185/2021.**


## PATA MKOPO

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).KWA MAWASILIANO ZAIDI

**TUPIGIE:0677 111 333**

**AU 0758 112 332**

**NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**


**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi**
**NO.282/2021**

Ombi la **TULIBWILA S. MWANGOSI** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **BEATUS GASPER KINYAGA** Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 12/10/2021** kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

**Tarehe 07/09/2021**

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA**
**WILAYA YA KINONDONI**
**MWANANYAMALA**
**SHAURI LA MADAI NAMBARI**
**817/835 LA 2021**
**SIMON NYATO............MUOMBAJI/WAOMBAJI**
**DHIDI YA**
**EDSON JUSTUS RWELAMIRA.........MDAIWA/WADAIWA**
**WITO KUITWA SHAURINI**
**EDSON JUSTUS RWELAMIRA – POPOTE ULIPO/MLIPO**

**SIMON NYATO** amefungua/wamefungua shauri mbele ya Baraza la Ardhi na Nyumba lililopo Kinondoni (Mwanyamala). Shauri husika limepangwa kutajwa/kusikilizwa **tarehe 29/09/2021 saa 3:00** asubuhi mbele ya Mh. L.R. Rugarabamu. Hivyo unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa.

Imetolewa na kutiwa saini na Mhuri wa Baraza hili leo tarehe 06 Mwezi 09 Mwaka 2021.


Kwa Habari Motomoto

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe


TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# G20 kuimarisha mpango wa COVAX nchi maskini

**Roma, ITALIA**

KUNDI la nchi 20 tajiri duniani (G20), limesema juhudi zaidi zinahitajika kuzisaidia nchi maskini kuchanja raia wao dhidi ya Covid-19, hazikueleza wazi idadi mpya ya dozi au ahadi za msaada wa kifedha.

Italia, ambayo ni mwenyekiti wa G20 mwaka huu, ilisema hayo baada ya mkutano wa Roma, juzi, kati ya mambo walioafikiana ni makubaliano ya kisiasa ili kuongeza msaada kwa nchi maskini na kuzipa chanjo zaidi.

"Kiwango cha ukosefu wa usawa katika ugavi wa chanjo ni cha juu sana na hali haiwezi kuendelea hivyo," Waziri wa Afya wa Italia Roberto Speranza aliwaambia waandishi wa habari.

"Ikiwa tutaiacha sehemu ya dunia bila chanjo, kuna hatari ya kukabiliwa na aina mpya ya virusi ambavyo vitatuathiri sote.

Ujumbe wetu uko wazi, hakuna yeyote wa kuachwa nyuma katika kampeni ya kutoa chanjo," aliongeza.

Chanjo zinasafirishwa kwenye nchi maskini kupitia mpango wa kimataifa wa COVAX, unaoungwa mkono na Shirika la Afya Duniani (WHO) na Mpango wa Chanjo na Kinga Duniani (GAVI).

*VOA*



Wanafunzi wakihudhuria masomo kwenye darasa katika mazingira mapya ya kuwa darasani Chuo Kikuu cha Avicenna mjini Kabul, nchini Afghanistan. **PICHA: REUTERS**

# Makabidhiano ya kwanza ya madaraka yafanyika Guinea

**Kankan na Labé, GUINEA**

HOTUBA ya dakika tano ya kiongozi mkuu wa mapinduzi Guinea, juzi, aliahidi kuunda serikali ya umoja wa kitaifa itakayohusika na kuongoza mabadiliko ya kisiasa, muda hakuutaja.

Jeshi limeanza kuchukua nafasi ya mamlaka ya raia na sheria ya kutotoka nje, kuanzia 4:00 usiku hadi saa 11:00 alfajiri.

Wakati huo huo, makabidhiano ya kwanza ya madaraka yalifanyika juzi katika mikoa ya Kankan na Labé.

Kankan, ngome ya Alpha Condé ambako Mamady Doumbouya anatoka, makabidhiano kati ya raia na wanajeshi yalifanyika wiki hii.

Gavana na mkuu wa wilaya wamebadilishwa. Kwa mujibu wa mashahidi kutoka mkoa huo, shughuli zilisitishwa ka muda katika jiji la Haute-Guinée kabla ya kuanza tena kama kawaida baadae mchana.

Kiongozi wa shirika la kiraia katika mkoa wa Kankan, Louncény Chérif, alielezea tukio lisilo kuwa la kawaida ambalo haikushabikiwa na watu wengi wala kupingwa kwa viongozi wapya, tofauti na wilaya zingine ambazo wanajeshi walilakiwa kwa vifijo na nderemo.

Alisema kuliripotiwa makundi madogo madogo ya watu, wakiongea kuhusu siasa na wengine, mbele ya redio zao, wakifuatia hotuba ya Mamady Doumbouya iliyorushwa moja kwa moja kutoka makao makuu ya Bunge huko Conakry.

Labé, katika eneo la Fouta Djalon, pia makabidhiano ya madaraka yalifanyika kati ya raia na wanajeshi. Lakini katika ngome hii ya chama cha UFDG, chama cha kiongozi wa pinzani Cellou Dalein Diallo, wakazi walikusanyika mbele ya jengo ambako sherehe ilifanyika kuelezea kuridhika kwao au hasira yao kwa gavana anayemaliza muda wake, kulingana na mashahidi kadhaa.

Hata hivyo, Jumuiya ya Maendeleo ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), itafanya mkutano wa dharura kesho, kujadili hali nchini Guinea ambako jeshi limetangaza kuchukua madaraka baada ya kuipindua serikali ya Rais Alpha Conde.

Mkutano huo wa viongozi wakuu wa kikanda umeitishwa siku moja tangu jumuiya hiyo kulaani hatua ya jeshi kuipindua serikali na kutaka kurejeshwa kwa utawala wa kikatiba au taifa hilo litawekewa vikwazo.

Tayari watawala hao walikwishatangaza kulivunja Bunge na kusitisha katiba ya taifa na juzi walifanya mabadiliko makubwa ya kiutawala kwa kuteua magavana wapya wa majimbo Guinea.

**RFI**

# Wasichana watembezwa utupu kufanya tambiko la mvua India

**Madhya Prades, INDIA**

WASICHANA sita wadogo katika eneo la kati mwa India walivuliwa nguo na kutembezwa katika maandamano wakiwa utupu, kama sehemu ya matambiko ya kuombea mvua.

Tukio hilo lilitokea katika kijiji kilichokumbwa na ukame katika eneo la Bundelkhand jimbo la Madhya Prades.

Video iliyosambazwa katika mitandao ya kijamii inaripotiwa kuwaonyesha wasichana wadogo, wakitembea utupu wakiwa wamewekelea fimbo ya mbao iliyokuwa imefungwa chura mabegani.

Wakazi wanaamini matambiko hayo yanawatukuza miungu wa mvua kuleta mvua katika eneo hilo.

Tume ya Kitaifa ya kulinda na kutetea haki za watoto India, imeitisha ripoti kutoka kwa mamlaka ya Wilaya ya Damoh, ambako kijiji hicho kinapatikana.

Polisi wa Madhya Pradesh, alisema hawajapokea malalamiko ya aina yoyote dhidi ya hafla hiyo na aliongeza kwamba, wameanzisha uchunguzi.

"Hatua itachukuliwa indapo itabainika kuwa wasichana hao walilazimishwa kutembea utupu," Mkuu wa polisi wa Damoh Dkt Teniwar aliambia shirika la habari Trust India.

Video inaonesha wasichana hao, baadhi yao wana umri mdogo wa hadi miaka mitano, wakitembea katika maandamano hayo, wakifuatiwa na kundi la wanawake wanaoimba nyimbo za kidini.

Msafara huo ulisimama katika kila nyumba ya kijiji hicho huku watoto wakikusanya nafaka za chakula, ambazo baadaye zilitolewa kama msaada wa jamii katika hekalu la eneo hilo.

"Tunaamini hii italeta mvua," PTI aliwanukuu wanawake waliokuwa katika maandamano hayo wakisema.

Mratibu wa Wilaya ya Damoh S Krishna Chaitanya alisema wazazi wa wasichana hao walitoa idhini washiriki katika ibada hiyo.

"Katika visa kama hivyo, uongozi unaweza tu kuwafanya wanakijiji kuelewa athari za ushirikina huo na kuwafanya waelewe kuwa vitendo kama hivyo havileti matokeo yanayotarajiwa," akaongeza.

Kilimo cha India kinategemea sana mvua za masika na katika mikoa mingi, kuna matambiko yanayofanywa kuwatukuza miungu kulingana na mila na desturi za huko.

Baadhi ya jamii zinafanya yagnas (matambiko ya moto ya Kihindu), wengine wanabeba vyura au punda wakishiriki ibada hiyo huku wakiimba nyimbo za kuwatukuza miungu wa mvua. Wakosoaji wanasema mila hiyo huwachanganya tu watu wa kawaida kutoka kwa ugumu, wataalam wa kitamaduni wanasema mazoea hayo ni ishara ya kukata tamaa kwa wale ambao wanaamini kuwa hakuna mahali pengine pa kutafuta msaada.

**BBC**

MECHI KALI
HOME
AWAY
POLAND
5.34 | 3.48 | 1.71
ENGLAND

1
WEKA PESA.
- PIGA *150*87#,
CHAGUA 4 - WEKA PESA.
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA halopesa

2
WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 482

# WILLIAN AFICHUA SIRI KUONDOKA ARSENAL



**RIO DE JANEIRO,** Brazil

KIUNGO wa Arsenal aliyeondoka na kurudi kwao Brazil, Willian amesema kwamba, hakuwa na furaha wakati wa kipindi chake cha kucheza kwenye kikosi cha Arsenal.

Willian aliondoka Chelsea akiwa ni miongoni mwa wachezaji wenye viwango vikubwa ndani ya klabu na kwenye Ligi Kuu England (EPL), wa ujumla.

Kujiunga kwake na 'Washikabunduki' hao, hakuna aliyetegemea kama angekuwa na wakati mgumu.

Maisha ndani ya Arsenal yalimwendea mrama nyota huyo wa Brazil na sasa ameondoka pale kwenye dimba la Emirates baada ya makubaliano ya kusitisha mkataba wake na kurudi katika Klabu ya Corinthians nchini Brazil.

Akizunguma na TV Corinthians, kiungo huyo ameamua kufunguka kilichotokea: "Nilifikiria sana, pamoja na familia na watu wangu wa karibu. Kwa bahati mbaya, muda wangu ndani ya Arsenal haukuwa mzuri, sikuwa na furaha.

"Sitaki kuliongelea sana kwa undani, lakini sikuwa na furaha na kurejea Brazili lilikuwa ni chaguo sahihi.

"Niliangalia fursa nyingi, lakini nilichagua kurejea Corinthians, nyumbani kwetu, niwe karibu na familia yangu. Ndio klabu iliyonitambulisha duniani, muda sahihi wa kurejea ulikuwa ni huu."

# SOUTHGATE: ENGLAND HAIMFIKIRII TU LEWANDOWSKI



**LONDON, England**

ENGLAND hawezi kujikita zaidi kwa kumfikiria Robert Lewandowski wakati wa mchezo wao wa leo Jumatano wa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia dhidi ya Poland, kocha wa 'Simba Watatu' hao, Gareth Southgate amewaonya wachezaji wake.

Lewandowski alifunga mara tatu katika ushindi wa Poland dhidi ya Albania na San Marino wiki iliyopita na kumfanya afikishe mabao 72 kwa nchi yake katika mechi 124.

Ameendeleza rekodi yake kutoka msimu wa 2020-21, wakati alipotengeza rekodi ya kufunga mabao mengi kwenye msimu mmoja wa Bundesliga (41), na amekuwa na kiwango bora msimu huu. Alifunga katika mechi zote sita kwa klabu na nchi yake, na straika huyo wa Bayern Munich aliumia wakati Poland walipofungwa 2-1 pale Wembley, Machi mwaka huu kwenye mchezo wa kundi hilo la I.

Lakini wakati akiwa anatambua kiwango kizuri cha Lewandowski, Southgate amesisitiza kuna vitu vingi zaidi kwa Poland na si mchezaji mmoja tu.

"Walicheza Wembley bila yeye na walionyesha kiwango cha kuvutia zaidi wachezaji wengine waliopo," alisema Southgate akiwaambia waandishi wa habari.

"Tulifunga katika muda wa majeruhi kuweza kupata ushindi, hivyo hauna tofauti na mchezo wa kesho (leo), kwani tunatakiwa kujipanga vizuri.

"Wana wachezaji ambao wanaipigania timu yao na sisi tuna wachezaji wazuri, hivyo tunakifikiria kikosi chote na siyo mchezaji mmoja."

,274,020

JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/21 | 17:00 | Brentford vs Brighton | 2.72 | 3.12 | 2.72 |
| 02. 11/09/21 | 17:00 | Watford vs Wolverhampton | 3.27 | 3.17 | 2.30 |
| 03. 11/09/21 | 17:00 | Southampton vs West Ham | 2.87 | 3.42 | 2.42 |
| 04. 11/09/21 | 17:15 | Ternana vs Pisa | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 05. 11/09/21 | 19:00 | Napoli vs Juventus | 2.56 | 3.46 | 2.66 |
| 06. 11/09/21 | 22:00 | Amorebieta vs Burgos | 2.42 | 2.95 | 3.10 |
| 07. 12/09/21 | 14:00 | Montpellier vs St Etienne | 2.44 | 3.38 | 2.79 |
| 08. 12/09/21 | 16:00 | Bordeaux vs Lens | 3.09 | 3.39 | 2.24 |
| 09. 12/09/21 | 16:00 | Brest vs Angers | 2.65 | 3.30 | 2.60 |
| 10. 12/09/21 | 16:00 | Spezia vs Udinese | 2.92 | 3.38 | 2.40 |
| 11. 12/09/21 | 17:15 | Osasuna vs Valencia | 2.51 | 3.07 | 3.02 |
| 12. 12/09/21 | 18:30 | VfL Bochum vs Hertha BSC | 2.93 | 3.23 | 2.41 |
| 13. 12/09/21 | 19:15 | Ponferradina vs Almeria | 2.80 | 3.30 | 2.41 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATANO - 08 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:30 | 1124 | FC Brasov vs Miercurea Ciuc | 3.15 | 3.25 | 2.13 |
| 16:30 | 1181 | Unirea Dej vs FCM Baia Mare | 1.83 | 3.44 | 3.88 |
| 16:30 | 1838 | Scolar Resita vs Ripensia Timisoara | 2.81 | 3.25 | 2.32 |
| 16:30 | 2565 | CF Braila vs Petrolul Ploiesti | 4.55 | 3.63 | 1.67 |
| 16:30 | 2616 | ACS CAO 1910 Oradea vs Universitatea Cluj | 3.58 | 3.44 | 1.91 |
| 16:30 | 3654 | Dunarea Calarasi vs Astra Giurgiu | 2.11 | 3.24 | 3.20 |
| 16:30 | 5969 | ACS Husana Husi vs FC Politehnica Iasi | 3.63 | 3.39 | 1.91 |
| 17:00 | 1942 | Unia Skierniewice vs MKS Kutno | 1.77 | 3.69 | 3.88 |
| 17:00 | 4257 | FC Dynamo-Makhachkala vs Skvo Rostov | 3.18 | 3.18 | 2.14 |
| 17:00 | 4431 | FC Vysocina Jihlava B vs Velke Mezirici | 2.35 | 3.78 | 2.47 |
| 17:30 | 2826 | Banik Ostrava B vs Uhersky Brod | 1.37 | 5.05 | 6.02 |
| 17:30 | 4595 | KS Korona Rzeszow vs Orleta Radzyn Podlaski | 2.23 | 3.59 | 2.72 |
| 17:30 | 5318 | Druzhba vs Biolog Novokubansk | 6.00 | 3.75 | 1.60 |
| 18:00 | 1325 | MKS Podlasie Biala Podlaska vs Podhale Nowy Targ | 3.53 | 3.58 | 1.88 |
| 18:00 | 1582 | Santiago Morning vs Copiapo | 2.47 | 3.10 | 2.72 |
| 18:00 | 1749 | SFK Vrchovina vs Blansko | 3.54 | 3.88 | 1.80 |
| 18:00 | 1850 | ZKS Unia Tarnow vs Siarka Tarnobrzeg | 3.48 | 3.72 | 1.86 |
| 18:00 | 1999 | LKS Lodz II vs Pilica Bialobrzegi | 2.27 | 3.52 | 2.70 |
| 18:00 | 3286 | Loko Vltavin vs Usti Nad Labem | 3.38 | 3.34 | 2.00 |
| 19:00 | 3633 | Armenia vs Liechtenstein | 1.14 | 7.63 | 18.07 |
| 19:00 | 4469 | Vinbergs IF vs Dalstorps IF | 1.89 | 3.96 | 3.19 |
| 19:30 | 1437 | Notvikens IK vs Bergnasets Aik | 2.19 | 3.54 | 2.81 |
| 19:30 | 3476 | Bulgaria vs Georgia | 1.86 | 3.59 | 4.09 |
| 20:00 | 2214 | Varbergs Gif FK vs Hoganas BK | 3.05 | 3.90 | 2.10 |
| 20:00 | 2620 | IK Oddevold vs IK Gauthiod | 1.30 | 5.24 | 7.38 |
| 20:00 | 2708 | Friska Viljor FC vs Gottne IF | 1.75 | 3.77 | 3.87 |
| 20:00 | 3244 | Eslovs BK vs BK Olympic | 4.05 | 3.67 | 1.74 |
| 20:00 | 4127 | Enkoping SK vs FC Arlanda | 1.64 | 4.07 | 4.17 |
| 20:00 | 4256 | Vastra Frolunda IF vs BK Astrio | 2.35 | 4.00 | 2.60 |
| 20:00 | 4326 | Solvesborgs Goif vs KSF Prespa Birlik | 2.38 | 3.62 | 2.51 |
| 20:00 | 4907 | FC Rosengaard vs Nosaby IF | 1.51 | 4.25 | 5.02 |
| 20:00 | 5241 | Umea FC Akademi vs Sandviks IK | 3.10 | 3.44 | 2.07 |
| 20:00 | 5277 | Mlks Wissa Szczuczyn vs Lechia Tomaszow Mazowiecki | 2.70 | 3.67 | 2.21 |
| 20:00 | 5413 | SV Seekirchen vs SV Kuchl | 2.81 | 3.78 | 2.11 |
| 20:00 | 5625 | Skiljebo SK vs Kungsangens IF | 1.38 | 5.05 | 5.83 |
| 20:30 | 1548 | Al Khaleej Club vs AL Jeel | 2.30 | 3.40 | 3.05 |
| 20:30 | 2189 | SV Hemelingen vs ESC Geestemunde | 2.41 | 4.35 | 2.22 |
| 21:30 | 5280 | Union La Calera vs Santiago Wanderers | 1.49 | 3.97 | 5.81 |
| 21:45 | 1323 | Belarus vs Belgium | 19.98 | 7.59 | 1.14 |
| 21:45 | 1409 | Kosovo vs Spain | 15.02 | 6.21 | 1.20 |
| 21:45 | 2226 | Hungary vs Andorra | 1.05 | 11.95 | 49.80 |
| 21:45 | 2508 | Poland vs England | 5.34 | 3.48 | 1.71 |
| 21:45 | 4076 | Iceland vs Germany | 11.64 | 5.73 | 1.25 |
| 21:45 | 4426 | Northern Ireland vs Switzerland | 5.20 | 3.45 | 1.73 |
| 21:45 | 4951 | Albania vs San Marino | 1.03 | 13.99 | 59.94 |
| 21:45 | 5089 | Italy vs Lithuania | 1.07 | 9.77 | 45.08 |
| 21:45 | 5763 | North Macedonia vs Romania | 2.54 | 3.24 | 2.79 |
| 21:45 | 5799 | Greece vs Sweden | 3.49 | 3.14 | 2.20 |
| 21:45 | 5954 | Wales vs Estonia | 1.18 | 6.61 | 16.02 |
| 23:30 | 5660 | Santos Guapiles vs AD San Carlos | 1.80 | 3.40 | 4.08 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.



# JORGINHO: NDOTO YANGU NI KURUDI TENA ITALIA

**LONDON,** England

KIUNGO wa Chelsea, Jorginho, amesema kwamba ana ndoto ya kurejea nchini Italia, kwa mujibu wa wakala wake, Joao Santos.

Mchezaji huyo ambaye alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mwaka wa kiume wa Shirikisho la Soka la Ulaya (UEFA), anafikiria kuondoka darajani pale mara baada ya mkataba wake kumalizika mwaka 2023.

Chelsea walilipa kiasi cha pauni milioni 50 kumnasa Jorginho kutoka Napoli wakati wa majira ya joto mwaka 2018 na kumfunga kwa mkataba wa miaka mitano.

Mkataba huo upo njiani kumalizika si zaidi ya miaka miwili na Santos amesema kwamba anaweza kuondoka Stamford Bridge kabla ya mwaka huo.

"Ana mkataba na Chelsea mpaka mwaka 2023," Santos aliiambia Radio Bianconera.

"Kimsingi itakuwa ni ndoto kwa Jorginho kurejea Italia baada ya kuwa na tumaini la kushinda Kombe la Dunia.

"Tutaangalia soko litakavyokuwa limekaaje kwa miaka miwili ijayo na hali nyingine zitakavyokuwa.



# BARCA YAMTAKA KOEMAN KUWATUMIA PUIG, UMTITI

**BARCELONA, Hispania**

RAIS wa Barcelona, Joan Laporta, amemtaka kocha wa klabu hiyo, Ronald Koeman, kuwapa nafasi ya kucheza Riqui Puig na Samuel Umtiti.

Koeman anaonekana kutokuwa na mipango mikubwa na Puig na Umtiti, huku akiwa na chaguo tofauti.

**Lakini Laporta anatamani wachezaji hao watumike zaidi kwenye kikosi cha Bar celona mwanzo wa kampeni hii ya Ligi Kuu Hispania, La Liga.**

Nyota hawa wawili hawakupokea ofa ambazo zilikubaliwa na mabosi wa Barcelona wakati wa msimu wa uhamisho, kuwapo kwao kulitarajiwa kuwa chachu ya mabadiliko klabuni hapo.

Hata hivyo, Puig na Umtiti, wote hawakupata muda wa kucheza Agosti wakati wa maandalizi ya msimu mpya, ikiwa ni ishara kuwa Koeman huenda hana mipango mikubwa na wachezaji hawa kwenye kikosi chake cha kwanza.

Lakini taarifa zinasema kuwa Laporta ana imani kubwa na wachezaji hawa ikiwa watatumiwa vizuri.

Kwa mujibu wa The Marca, Laporta anataka kocha Koeman awatumie vizuri Puig na Umtiti kwa kipindi chote cha msimu kilichosalia.

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# VAN DE BEEK ATULIZWA MZUKA KUONDOKA UTD

●●● Kama huchezi, jaribu kuwasaidia wao, kuna wakati unaweza kukaa pale na kuwa na hasira, lakini hilo si...

**ENGLAND**

DONNY van de Beek sasa ana matumaini ya kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha Manchester United baada ya kufanya mazungumzo mazuri na kocha wake, Ole Gunnar Solskjaer - ingawa amekiri kwamba, muda wake nchini England umekuwa "ni mgumu sana."

Alisajiliwa kutoka Ajax Septemba mwaka jana kwa ada ya awali ya pauni milioni 34.7 na mchezaji huyo wa kimataifa wa Uholanzi, alifunga bao lake la kwanza kwenye Ligi Kuu England katika mchezo wa nyumbani, dhidi ya Crystal Palace.

Tangu hapo kiungo huyo amekuwa na wakati mgumu wa kupata nafasi ya kucheza kwenye kikosi cha kwanza.

Ameanza katika mechi nne tu za Ligi Kuu kwa 'Mashetani Wekundu' hao, akicheza kwa dakika 1,460, chache zaidi kuliko walinzi wa ziada, Eric Bailly na Alex Telles.

Wakala wa Van de Beek alibainisha kwamba, kulikuwa na nafasi ya yeye kujiunga na Everton wakati wa dirisha la uhamisho wa majira ya joto lililopita, huku usajili wa Jadon Sancho na Cristiano Ronaldo ukiongeza ufinyu wa yeye kupata nafasi ya kucheza, lakini hakukuwa na ofa yoyote.

Sasa, Van de Beek amesema Solskjaer amemuweka wazi kuhusu nafasi yake ya kucheza, ingawa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, hajapata nafasi ya kuichezea United msimu huu.

Akizungumza na Vibe with Five, alisema: "Mwaka wa kwanza, unakuja kutoka mashindano mengine na ni kawaida unahitaji kuzoea mazingira. Lakini bila shaka, unakuwa huna furaha. Nataka kucheza, ni hilo tu.

"Ni ngumu sana. Bila shaka, pia kiakili, ni ngumu sana. Kitu pekee unachoweza kufanya ni kujifua kila siku kwa bidii na kujaribu kujiimarisha na kusubiri nafasi ya kucheza.

"Kama nafasi inakuja natakiwa kuwa tayari. Kama umepoteza au vyovyote, ni suala la kuzungumza tu na wachezaji, kuwa sehemu ya timu.

"Kama huchezi, jaribu kuwasaidia wao kuwa katika mtazamo chanya. Unaweza kukaa pale na kuwa na hasira, lakini hilo si suluhisho.

"Unahitaji kuhusika na timu moja kwa moja. Kuna wakati unakuwa na hasira kwa kila mchezaji mwenzako.

"Unataka kuwaonyesha kwamba unafanya mazoezi kwa bidii kubwa na kujituma sana, ili umpe kocha nafasi ya kukupanga, lakini hakuna kinachotokea na hilo linakuwa jambo gumu sana kwa mchezaji.

"Nimezungumza na kocha kuhusu hilo pamoja na klabu na walikuwa wazi kwamba, wanataka mimi nibaki.

"Kocha alikuwa na mtazamo chanya kuhusu mimi na alisema 'nakuhitaji wewe, nataka kukubakiza hapa kwa sababu kile nilichokiona kwenye mazoezi, namuona Donny tofauti'. Alikuwa sahihi kabisa kwangu."

## ZISIKUPITE

### RICE BADO ATAKIWA UNITED

MANCHESTER United bado wanamtaka mchezaji wa West Ham, Declan Rice mwenye umri wa miaka 22, ingawa hawakumnunua msimu huu wa majira ya joto. **(ESPN)**

### ASENSIO NDANI RADA LIVER

LIVERPOOL pia inamtaka mshambuliaji wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 25, ambaye anajiandaa kuondoka Real Madrid. **(Todofichajes)**

### VAN DE BEEK KWENDA EVERTON

WAKALA wa kiungo wa kati wa Manchester United, Donny van de Beek amesema amefanya mazungumzo na Everton kuhusu uwezekano wa uhamisho wa mchezaji huyo wa Uholanzi mwenye umri wa miaka miaka 24. **(Express)**

### PSG WAMTAKA KASSIE

PSG wameelekeza darubini yao kwa kiungo wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie mwenye umri wa miaka 24, kwani wanaamini mchezaji wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba mwenye miaka 28, angelipendelea kuhamia Real Madrid msimu ujao. **(Defensa Central)**

### ELNENY AGONGA MWAMBA

PENDEKEZO la kiungo wa Arsenal, Mohamed Elneny kuhamia Besiktas limegonga mwamba kutokana na matakwa ya hali ya juu ya marupurupu anayotaka mchezaji huyo wa Misri mwenye umri wa miaka 29. **(talkSPORT)**

### SOLER AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL wanatafakari uwezekano wa kumsajili kiungo wa kati wa Valencia na Hispania, Carlos Soler, ambaye ana kifungu cha kutolewa cha pauni milioni 125 katika mkataba wake. Kocha wa Reds Jurgen Klopp anataka Soler kuchukua nafasi ya kiungo wa kati wa Uholanzi, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, ambaye alijiunga na Paris St-Germain kama mchezaji huru. **(Fichajes)**

### RAMSEY AKATAA KUONDOKA JUVE

KIUNGO wa Wales, Aaron Ramsey mwenye umri wa miaka 30, amekataa ofa kadhaa za kuondoka Juventus wakati wa msimu wa majira ya joto, kwani anatarajia kuwa katika kikosi cha kwanza chini ya kocha, Massimiliano Allegri. **(Calciomercato)**

### FODEN MKATABA MPYA

PHIL Foden mwenye umri wa miaka 21, anajiandaa kupewa ofa ya mkataba mpya na Manchester City licha ya kiungo huyo wa England kubakiza miaka mitatu katika mkataba wake wa sasa. **(Manchester Evening News)**

### MARTINEZA AWINDWA ATLETICO

KLABU ya Atletico Madrid huenda ikachukua hatua ya kumsajili kipa wa Argentina mwenye umri wa miaka 29, Emiliano Martinez kutoka Aston Villa ikiwa mchezaji wa kimataifa wa Slovenia, Jan Oblak mwenye miaka 28 ataagana na mabingwa hao wa LaLiga msimu ujao wa majira ya joto. **(La Razon)**

### PSG YAMFUKUZIA HERNANDEZ

KLABU ya Manchester City na PSG zinamfuatilia kwa karibu beki wa kushoto wa AC Milan na Ufaransa, Theo Hernandez mwenye umri wa miaka 23. **(Calciomercato)**

### SPURS NAO KWA KASSIE

KLABU ya Tottenham Hotspur, pia wanamtaka Franck Kessie na huenda wakamuuza kiungo wao wa kati wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 24, Tanguy Ndombele, ili kufanikisha ndoto hiyo. **(Express)**

## Biashara matumaini kibao kwa Wajibouti

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha timu ya Biashara United ya Mara, kinaondoka nchini leo, kuelekea Djibouti, kikiwa na matumaini makubwa ya kufanya vizuri dhidi ya wenyeji wao, FC Dikhil katika mchezo wa hatua ya awali ya Kombe la Shirikisho Afrika, CAF.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Patrick Odhiambo, alisema ana imani kubwa ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa ugenini baada ya kuona ubora na udhaifu wa wapinzani wao wanapokuwa nyumbani.

Alisema kwa kuwaangalia wapinzani wao hao na maamdalizi waliyoyafanya ya kujiandaa na msimu mpya, ana matarajio makubwa ya kufanya vizuri na kurejea na matokeo chanya.

"Tuko sawa, tumefanya maandalizi ya kutosha licha ya kutopata mechi za kirafiki za kimataifa. Tumecheza na timu za nyumbani na kupata mazoezi makubwa, kuwapo kwa wachezaji wa kimataifa wenye uzoefu wa michuano hii itatusaidia kupata matokeo katika mechi yetu hiyo," alisema Odhiambo akiwataja Ramadhani Ridondo 'Chombo' aliyewahi kupita Simba na Baron Okech Onyango, Opare Collins pamoja na Odongo Tayo waliowasajili kutoka nje ya nchi. Biashara United, ambayo inashiriki michuano hiyo ya kimataifa kwa mara ya kwanza itashuka dimbani keshokutwa Ijumaa kabla ya timu hizo kurudiana Uwanja wa Benjamin Mkapa Septemba 18, mwaka huu.

## New Generations Queens na sababu kutolewa CAF

**Na Hawa Zanzibar**

KOCHA Mkuu wa timu ya New Generations Queens, Abdul-Mutik Haji 'Kocha Kiduu', amesema kuwapo kwa timu chache zinazoshiriki Ligi Kuu Zanzibar kwa Wanawake, ni moja ya sababu ya kufanya vibaya katika michuano ya Ligi ya Mabingwa barani Afrika kuwania tiketi ya kufuzu kwa Ukanda wa CECAFA.

Akizungumza na gazeti hili, kocha huyo alisema uchache wa timu pamoja na madaraja ya wanawake, yanasababisha wachezaji kutopata mechi nyingi na hata kukosa upinzani katika ligi.

Alisema kupitia michuano hiyo ameona timu nyingi zilizoshiriki zina muundo mzuri wa ligi nchini kwao mpaka kufikia hatua ya kumpata bingwa na zile zinazoshuka daraja.

"Mashindano yalikuwa mazuri, kwa jinsi tulivyo hapa nyumbani wachezaji wamejitahidi kadri ya uwezo wao kupambana licha ya changamoto nyingi za kutokuwa na maandalizi kwa timu yangu ikiwamo kupata mechi nyingi za kirafiki kutoka nje ya Zanzibar," alisema.

Aidha, alisema changamoto ya umaskini au kukosa fedha za kufanya usajili mzuri, pia imechangia kutokuwa na kikosi cha kupambana katika michuano hiyo mikubwa, ambayo timu yake ilipoteza mechi zote tatu za hatua ya makundi.

# YANGA KUPIGA TENA YA KIRAFIKI IKIISUBIRI RIVERS UTD

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

HUKU ikitarajia kucheza mechi moja ya kirafiki kabla ya Jumapili kuikaribisha Rivers United ya Nigeria kwenye mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Klabu ya Yanga imesema malengo yake ni kutinga hatua ya makundi ya michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF.

Yanga, ambayo imeshacheza mechi nne za kirafiki hadi sasa, ambazo ni dhidi ya Zanaco ya Zambia, DTB, Friend Rangers na Pan Africans, imeeleza kuwa inatarajia kupata mchezo mwingine mmoja kabla ya kuwavaa Wanaigeria hao katika Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili, jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema Kocha Mkuu wa timu hiyo, Nasreddine Nabi, ameuagiza uongozi kukitafutia kikosi chake mchezo mmoja wa kirafiki kabla ya Jumapili.

"Kocha amesema wiki hii tutakuwa na mchezo wa mwisho wa kirafiki, ambao utatupa picha halisi kuelekea katika mchezo wetu wa kimataifa,"alisema Bumbuli.

Alisema timu hiyo inaendelea vizuri na mazoezi na kila mchezaji akiwa na morali ya kufanya vizuri katika mchezo huo wa Ligi ya Mabingwa, ambao waanzia nyumbani.

Wakati huo huo, Msemaji wa klabu hiyo, Haji Manara, amesema kutinga hatua ya makundi ndiyo lengo mama na baada ya hapo wataangalia kinachofuata mbele.

Manara alisema: "Tunajiandaa ndani na nje ya uwanja. Ndani ikiwa na maana ya uwanjani na nje ikiwa na maana kuutangaza na kuhamasisha mashabiki wajazane uwanjani kuipa sapoti timu yetu, lengo letu la kwanza msimu huu ni kutinga hatua ya makundi. Baada ya hapo tutaangalia nini kinaendelea mbele, lakini kwanza kabisa makundi."

Kuhusu maandalizi ya mchezo huo, alisema yanaendelea vema na wanachotaka kufanya Jumapili si kupata ushindi tu, bali ushindi mnono, ambao utawaweka vizuri kuelekea kwenye mechi ya marudiano nchini Nigeria.

"Lengo si kupata ushindi tu, ila ushindi mnono ili kujiweka vema na mechi ya marudiano. Nimeona watu wanauliza kama mechi itakuwa na watu au watazuiwa kama ilivyokuwa kwenye mechi ya Taifa Stars na Madagascar, lakini ninavyojua ni kwamba mechi za kufuzu Kombe la Dunia zinasimamiwa na FIFA ambao wanazuia mashabiki, ila za Ligi ya Mabingwa zinasimamiwa na CAF. Nadhani wao hata kama watazuia, lakini wataruhusu idadi fulani ya mashabiki kuingia," alisema msemaji huyo.

**MSHINDI...**




Meneja wa Benki ya Exim Tawi la Zanzibar, Mwinyimkuu Ngalima (kushoto), akikabidhi zawadi kwa mshindi wa tatu upande wa wanaume kwenye mashindano ya CEO Golf 2021, Jacques Els. Benki ya Exim ilikuwa miongoni mwa wadhamini muhimu wa mashindano hayo yaliyofanyika mwishoni mwa wiki visiwani Zanzibar. **MPIGAPICHA WETU**

## Simba Queens kusukwa upya

**Na Somoe Ng'itu, NAIROBI**

BAADA ya timu yake kupoteza mchezo wa hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Ukanda wa Cecafa, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Hababuu Ali, amesema kikosi hicho kinahitaji kuimarishwa, kwa ajili ya kupambana zaidi kwenye michuano hiyo hapo mwakani.

Hata hivyo, juzi Simba Queens ikikabidhiwa kitita cha Dola za Marekani 15,000 kutoka kwa klabu baada ya kufika hatua ya nusu fainali ya michuano hiyo inayofanyika kwa mara ya kwanza barani Afrika.

Akizungumza na gazeti hili jana jijini hapa, Hababuu alisema mbali na kujipanga kwa ajili ya msimu ujao, Simba Queens, pia inatakiwa kuwa imara, ili kuhakikisha inatetea ubingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania.

Kocha huyo alisema dirisha la usajili Tanzania limefungwa, lakini atalazimika kuongeza nguvu wakati dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa, kwa ajili ya kupata wachezaji watakaomsaidia kuipaisha timu hiyo katika mashindano ya ndani na nje.

"Tumejifunza na tunarudi nyumbani kujipanga, pia tulikuwa tunacheza na wenzetu, ambao walikuwa wanaogopa jina la Simba, sasa tumepata mwanga na tutajipanga, kwa ajili ya kushindana kwa kiwango cha juu ili tupate nafasi ya kushiriki tena mwakani," alisema Hababuu.

Aliongeza kuwa wapinzani wao Vihiga Queens, walicheza kwa kujihami zaidi na nyota wake walifunguka ingawa hawakupata nafasi ya kufunga katika nafasi mbalimbali walizotengeneza.

Simba Queens sasa itashuka uwanjani kesho kucheza mechi ya kusaka mshindi wa tatu dhidi ya Lady Doves FC ya Uganda wakati Vihiga Queens watawakabili Commercial Bank of Ethiopia katika fainali ya michuano hiyo inayodhaminiwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan.

# Michezo

Jumatano Septemba 8, 2021

Nipashe




Van de Beek atulizwa mzuka kuondoka Utd UKURASA 22

HATUPOI...



Mfungaji wa bao la kwanza la Taifa Stars, Erasto Nyoni (kushoto), akipongezwa na Mbwana Samatta (katikati) pamoja na kiungo aliyeifungia bao la ushindi dhidi ya Madagascar, Feisal Salum 'Fei Toto' kwenye mechi ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia Qatar 2022. Katika mechi iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jana, Stars ilishinda 3-2. **MPIGAPICHA WETU**

# STARS KILELENI TIKETI KOMBE LA DUNIA 2022

## ●●● Samatta, Msuva kiwango juu wakati Nyoni, Novatus, Fei Toto wakiinyoa Madagascar huku...

**Na Adam Fungamwango**

KIWANGO bora kilichoonyeshwa na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta pamoja na mshambuliaji Simon Msuva, kilikuwa chachu ya ushindi wakati Erasto Nyoni, Dismas Novatus na Feisal Salum 'Fei Toto', wakiifungia timu hiyo mabao 3-2 dhidi ya Madagascar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jana.

Kwa ushindi huo Taifa Stars sasa inakaa kileleni mwa msimamo wa Kundi J, kwenye kinyang'anyiro cha kusaka tiketi ya kufuzu fainali za Kombe la Dunia mwakani nchini Qatar, lakini ikiwa na pointi sawa na Benin pamoja na tofauti ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Sekunde ya 10 tu, Taifa Stars ilifanikiwa kupata penalti baada ya Simon Msuva kuangushwa ndani ya eneo la hatari na golikipa Melvin Adrian. Alikuwa ni Nyoni aliyekwenda kupiga penalti hiyo na kuukwamisha mpira wavuni, dakika ya pili ya mchezo.

Dismas Novatus, aliipatia Taifa Stars bao la pili dakika ya 25, baada ya kuwapokonya mpira wachezaji wa Madagascar waliokuwa wanapasiana, akavuta hatua kadhaa na kupiga shuti hafifu lililokwenda kugonga nguzo ya pembeni na kujaa wavuni.

Ni kama wachezaji wa Stars waliona mechi imekwisha. Wakapunguza kasi yake ya mwanzo, hivyo kuwapa fursa wapinzani wao kushambulia.

Krosi iliyoonekana haina madhara iliyopigwa na Ibrahim Amada, iliwapita mabeki wa Stars, ikamkuta mchezaji aliyetokea benchini kipindi cha kwanza, Njiva Rakotoharimalala na mpira ukajaa wavuni.

Baada ya bao hilo wachezaji wa Stars walionekana kama wamechanganyikiwa, huku Madagascar wakicheza kandanda safi. Haikushangaza dakika ya pili ya nyongeza kabla ya kwenda mapumziko kusawazisha.

Alikuwa ni Thomas Fontaine aliyepiga faulo maridadi, iliyowapita kichwani mabeki wa Stars waliokuwa wameweka ukuta. Licha ya kipa Aishi Manula kuchupa kutaka kuuokoa, mpira huo ulikuwa umeshajaa wavuni.

Mwanzoni mwa kipindi cha pili Stars ilionekana kuchangamka, Samatta alibadilisha namba kutoka kati na kwenda pembeni. Hiyo ilimsaidia kuwahangaisha mabeki wa Madagascar.

Ilikuwa ni dakika ya 52, nahodha huyo alipoupata mpira kwenye winga ya kushoto na kuwahadaa mabeki wa timu pinzani, akapiga krosi pasi kwenda kwa Fei Toto, aliyetupia nyavuni na kuandika bao la tatu ambalo lilidumu hadi mwisho wa mchezo, licha ya kuonekana kuzidiwa mwishoni mwa kipindi cha pili, ambapo wageni walionekana kutafuta japo sare kwa udi na uvumba.

Kwa matokeo hayo, Stars sasa iko juu ya msimamo ikiwa na pointi nne, sawa na Benin iliyotoka sare ya bao 1-1 dhidi ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo juzi.

Mabao manne iliyokuwa nayo yameifanya kuwa kinara wa kundi, licha ya kufungwa mabao matatu, huku Benin ikiwa imefunga mabao mawili na kufungwa moja.

DR Congo, ikiwa nafasi ya tatu na pointi mbili na Madagascar ikiburuza mkia ikiwa haina pointi, kwani kwenye mechi ya kwanza ilichapwa bao 1-0 nyumbani dhidi ya Benin.

# Simba yaitaka Tusker ikiisubiri TP Mazembe

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

NI rasmi sasa Klabu ya Simba itajaribu mitambo yake na kutoa burudani kwa mashabiki na wanachama wao, itakaposhuka katika Uwanja wa Benjamin Mkapa dhidi ya TP Mazembe ya DR Congo, kucheza mechi ya kirafiki katika kikele cha Tamasha la Simba Day.

Katika kujiandaa na tamasha hilo linalotarajiwa kufanyika Septemba 19, mwaka huu, Simba imepanga kupata mechi moja ya kirafiki ya kimataifa ikiwa jijini Arusha, huku ikielezwa mipango inafanyika kucheza na Tusker FC ya Kenya.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema katika kuadhimisha Simba Day, timu hiyo itacheza na mabingwa mara tano wa Ligi ya Mabingwa Afrika, TP Mazembe.

Alisema wamekamilisha taratibu zote za kuwaalika na sasa ni rasmi TP Mazembe ya DR Congo, watakuwa wageni wa Simba siku hiyo muhimu ya kilele cha tamasha lao.

"Nifuraha kuwatangazia Wanasimba na Watanzania wote kwa ujumla kwamba tutacheza na TP Mazembe Simba Day, ni moja ya timu zenye heshima kubwa barani Afrika pia ni heshima kwa Simba kupata fursa ya kucheza nayo hapa nchini," alisema Gonzalez.

Alisema lilikuwa lengo la uongozi na benchi la ufundi kuhakikisha Simba inapata timu nzuri ili Kocha Mkuu, Didier Gomes kujua upungufu na ubora wa kikosi chake kuelekea msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania na Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema wachezaji wote 21 waliopo kambini jijini Arusha wako kwenye hali nzuri na wale wageni wamezoeana na wenzao pamoja na mazingira ya timu. Alisema waliendelea na mazoezi ya mara mbili kwa siku, asubuhi na jioni na kwamba kikubwa kwao ni kuendelea kutafuta stamina pamoja na mbinu za uwanjani kwa muda ambao watakuwapo kambini hapo huku wakitarajia kucheza mechi za kirafiki.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31

9 770856 541002 >